



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

**RIPOTI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA
KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA
TAREHE 30 JUNI 2020**

Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi

Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa

Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unapatikana katika matumizi mazuri ya rasilimali za umma Afisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:-

Uaminifu

Kuhakikisha Ofisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia sheria.

Uadilifu

Kuwa ni Ofisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

Kuwa Huru

Kuwa ni Ofisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa sheria

Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi

Kuwa ni Ofisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

Kutunza Siri

Kuwa ni Ofisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

Uwazi na Uwajibikaji

Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma.

YALIYOMO

MUHTASARI	1
SURA YA KWANZA	3
1.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA FEDHA (IFMIS) KATIKA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO - IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI	3
1.1 UTANGULIZI	3
1.2 MALENGO YA UKAGUZI	3
1.3 UPEO WA UKAGUZI	4
1.4 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI.....	5
1.5 CHANGAMOTO ZA UKAGUZI.....	5
1.6 MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO	6
SURA YA PILI	26
2.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA BODI YA MAPATO ZANZIBAR – ZRB.....	26
2.1 UTANGULIZI	26
SURA YA TATU	37
3.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO MKUU WA USIMAMIZI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR - PBZ.....	37
3.1 UTANGULIZI	37
SURA YA NNE	39
4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA BIASHARA SHIRIKA LA UMEME -ZECO	39
4.1 UTANGULIZI	39
SURA YA TANO	42
5.0 RIPOTI YA MFUMO WA USIMAMIZI WA TAARIFA NA MICHANGO YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII - ZSSF	42
5.1 UTANGULIZI	42
MAPENDEKEZO	44
VIAMBATISHO.....	45

MUHTASARI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua kuwa utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni moja kati ya sekta muhimu kwa ukuwaji wa haraka wa kiuchumi na hupelekea maendeleo makubwa kwa jamii.

Hii inadhihirishwa na mipango mbalimbali ya TEHAMA iliyochukuliwa na vyombo vya Serikali ili kuimarisha ufanisi wa utendaji wa kazi kwa gharama nafuu katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hutumia mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao ya kazi na biashara ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa ufanisi, weledi na kwa wakati.

Hata hivyo, baada ya ukaguzi kupitia mifumo iliyowekwa katika taasisi mbali mbali za Serikali imebainika kwamba baadhi ya mifumo inayotumiwa na Taasisi haikuratibiwa na kusimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha mifumo hiyo inaleta tija na ufanisi katika maendeleo ya Taasisi na Serikali kwa lengo la kupatikana thamani ya uwekezaji wa mifumo hiyo.


Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo makuu yanayotokana na ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA uliofanyika kwa ya Taasisi tano (5) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo ni Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Bodi ya Mapato Zanzibar , Benki ya Watu wa Zanzibar , Shirika la Umeme Zanzibar na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar. Ukaguzi huo ulilenga kuhakikisha kwamba ufanisi mkubwa wa utendaji kupitia mifumo hiyo unapatikana kwa kuzingatia sheria , Sera, Miongozo na taratibu bora zilizopangwa na zinazokubalika katika usimamizi wa mifumo ya TEHAMA.

Ukaguzi uliofanywa umeangalia usahihi na usalama wa taarifa zilizomo katika mifumo ya TEHAMA kwa kuzingatia usiri na udhibiti wa taarifa, uadilifu na usalama pamoja na upatikanaji wa taarifa kwa lengo la kuleta tija na ufanisi katika matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

Ripoti hii ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA inaelezea dosari zilizobainika, athari zinazotokana na dosari hizo, mapendekezo pamoja na hitimisho kwa taasisi tano (5) zilizokaguliwa mifumo ya TEHAMA ikiwemo Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Fedha, Mifumo ya Usimamizi wa Kodi, Mifumo ya Usimamizi wa Benki , Mifumo ya Usimamizi wa Biashara na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa na Michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

Dosari zilizobainika katika ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi hizo zimebainishwa katika sehemu mbali mbali kuanzia **Sura ya Kwanza** hadi **Sura ya Tano** ya ripoti hii.

Ni imani yangu kwamba dosari zote zilizobainika zitafanyiwa kazi kwa mujibu wa sera , miongozo ya Taasisi na Serikali pamoja na viwango vya kimataifa ili kuongeza udhhibiti na usalama katika usimamizi wa taarifa zilizomo ndani ya Mifumo ya TEHAMA ya Taasisi za Serikali.



.....
Dkt. OTHMAN ABBAS ALI

**KAIMU MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
ZANZIBAR**

SURA YA KWANZA

1.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA FEDHA (IFMIS) KATIKA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO - IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

1.1 UTANGULIZI

Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMIS) ni mfumo ambao umetengenezwa na kuwekwa katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa lengo la kusimamia taarifa za fedha za Serikali kuanzia hatua ya utayarishwaji wa bajeti ya Serikali, utekelezaji wa bajeti pamoja na utoaji wa ripoti za fedha za mapato na matumizi katika Mawizara, Idara, Wakala na Sekta za Umma.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imeanzisha mfumo wa IFMIS ikiwa ni hatua moja wapo ya maendeleo ya matumizi ya TEHAMA katika kuimarisha utoaji wa huduma za fedha na kuongeza ufanisi, udhibiti, uwajibikaji, uwazi, usalama wa taarifa za fedha pamoja na utoaji wa taarifa za bajeti na taarifa za fedha.

Mfumo wa IFMIS umetengenezwa na kampuni ya **Soft Tech Consultants Ltd (STCL)** na unatumia programu ya **EPICOR VERSION 10.1.4.** ambao unaweza kuunganishwa na mifumo mengine ya TEHAMA kwa vile mfumo huo unafanya kazi katika mazingira (Platform) ya **Window Based Operating System.**

Mfumo huu umegawika katika moduli mbali mbali ikiwemo moduli ya wanaodai, moduli ya wanaodaiwa, moduli ya manunuzi, moduli ya mali za kudumu, moduli ya Daftari kuu la uhasibu, moduli ya usimamizi wa fedha taslim pamoja na moduli ya manunuzi mtandaoni.

Mfumo huo umeunganishwa na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA ikiwemo Seva, Kompyuta, vifaa vya mtandao, printa, skana n.k. ambavyo vinasaidia katika utoaji taarifa zilizo sahihi na kwa wakati juu ya hali ya kifedha ya Serikali.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kupitia kitengo chake cha TEHAMA kilifanya uboreshaji wa matumizi bora ya TEHAMA ilikuongeza ufanisi na uwajibikaji katika matumizi ya Mfumo wa IFMIS. Kitengo hicho kilitengeneza Sera za TEHAMA ikiwa ni zana muhimu ya kuhakikisha matumizi bora ya TEHAMA na mfumo katika kusaidia utekelezaji wa shughuli za kila siku.

1.2 MALENGO YA UKAGUZI

Ukaguzi huu wa mfumo wa IFMIS ulifanywa kutokana na maombi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango yaliyowasilishwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia barua namba DC.184/199/01/03/81 ya tarehe 8 Februari 2021.

Malengo ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini udhibiti na usalama wa mfumo wa IFMIS kwa kuweza kupima kiwango cha utunzaji wa siri, uadilifu, ufanisi na urahisi wa upatikanaji wa taarifa za fedha zilizomo ndani yake pamoja na kuangalia usalama wa miundombinu ambayo mfumo huo umehifadhiwa.

Malengo hayo yamefanikiwa kwa kuangalia maeneo yafuatayo:-

1.2.1 Udhibiti wa Jumla (General Controls)

- Muundo na Usimamizi wa sera za TEHAMA na miongozo mengine,
- Udhibiti wa matumizi ya TEHAMA (IT operation Controls),
- Udhibiti wa nje wa miundombinu ya TEHAMA (Physical Access control)
- Udhibiti wa ndani wamiundombinu ya TEHAMA (Logical Access Controls)
- Udhibiti wa Muendelezo wa Biashara na Kupona Maafa (Business Continuity and Disaster Recovery Controls),
- Mgawanyo wa majukumu kwa wafanyakazi wa TEHAMA,
- Usimamizi wa Mipangilio (Configuration Management).

1.2.2 Udhibiti wa Mfumo (Application Controls)

- Udhibiti juu ya uingizaji wa taarifa/miamala ndani ya mfumo,
- Udhibiti juu ya uchakataji wa taarifa,
- Udhibiti juu ya utoaji wa ripoti, na
- Udhibiti juu ya taarifa zilohifadhiwa na mfumo na majalada makuu (Controls over standing data and master files).

1.2.3 Udhibiti Maalum

- Udhibiti wa mitandao ikiwemo vihatarishi vinavyohusika na udhibiti wa mitandao.
- Sera za usalama wa TEHAMA.
- Mapitio ya mikataba inayohusika na huduma za TEHAMA.
- Kuwafikiana na viwango (Compliance).

1.3 UPEO WA UKAGUZI

Ukaguzi huu umefanyika kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa (e-Goz na COBIT).

Ukaguzi huu umejikita zaidi juu ya mifumo ya habari na taratibu za kiusalama zinazotumiwa na Idara ya Mhasibu Mkuu - IFMIS katika utayarishaji wa taarifa za hesabu.

1.4 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi ulipata uelewa wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha kwa kupitia njia ya majadiliano na uchunguzi pamoja na ukaguzi wa nyaraka mbalimbali ikiwemo Sera za TEHAMA, miongozo na taratibu nyengine za Wizara. Katika kufanya ukaguzi huu hatua zifuatazo zilitumika:-

- Kukusanya taarifa na kufanya mahojiano na wahusika.
- Kupitia miundombinu ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha wa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (IFMIS);
- Kufanya tathmini ya vihatarishi vya mfumo wa IFMIS, mazingira ya kiusalama na programu na kutayarisha mpango wa ukaguzi uliozingatia tathmini hiyo.
- Kufanya majaribio mbali mbali ya kupima kwa viwango ili kuona kwa kiasi gani udhibiti na taratibu ziliziwekwa zinafanya kazi kama zilivyokusudiwa. Vilevile, tumetumia sampuli zilizochaguliwa na wakaguzi katika kukamilisha majaribio yetu ya kufikia viwango.
- Sheria, kanuni na viwango mbali mbali vya kitaifa na kimataifa vilitumika katika kufanya tathmini ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha wa Idara ya Mhasibu Mkuu (IFMIS) .

1.5 CHANGAMOTO ZA UKAGUZI

Wakati tunafanya ukaguzi huu tuliomba baadhi ya taarifa za kifedha kutoka idara ya Hazina - kitengo cha Exchequer kwa lengo la kutathmini usahihi na ukamilifu wa ripoti za kifedha zinazozalishwa na mfumo wa IFMIS, ili kuweza kujiridhisha kama mfumo unaisaidia Serikali katika kuhakikisha uwajibikaji na uwazi unakuwepo katika ukusanyaji wa mapato, matumizi ya fedha za umma pamoja na utoaji wa ripoti zake.

Hata hivyo ukaguzi haukupatiwa taarifa hizo za fedha zilizoombwa kutoka kitengo cha Hazina ikiwemo taarifa za hesabu za kitengo cha Exchequer za ukusanyaji wa mapato, taarifa za hesabu za kitengo cha Exchequer zinazotumika kufanya malipo (mbali ya zile zilizounganishwa katika mfumo wa IFMIS), taarifa za mwaka za mapato kwa mujibu wa aina ya mapato kwa miaka mitatu iliyopita 2017/2018 – 2019/2020, taarifa za mwaka za matumizi za hesabu za benki ambazo hazijaunganishwa na

mfumo wa IFMIS kwa miaka mitatu iliyopita na bakaa za benki za hesabu zote za kitengo cha Exchequer hadi mwisho wa mwaka wa fedha kwa miaka mitatu iliyopita.

Kutokana na kukosekana kwa taarifa zilizoombwa hapo juu, ukaguzi umeshindwa kulinganisha iwapo taarifa zilizoripitiwa katika Hesabu Jumuishi za Serikali zinaendana na taarifa halisi za kifedha zinazozalishwa na mfumo wa IFMIS.

Hivyo ukaguzi umeshindwa kutoa maoni juu ya usahihi na ukamilifu wa taarifa za kifedha zilizoripitiwa katika Hesabu Jumuishi za Serikali kwa kutumia Mfumo wa IFMIS, ikiwemo mapato yaliyoripitiwa kukusanywa na matumizi yaliyoripitiwa kutumika na Hazina pamoja na bakaa za fedha za kitengo cha Hazina mwishoni mwa miaka ya fedha.

1.6 MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

Dosari zilizobainika katika ukaguzi huu zimeelezwa kwa njia tofauti kama vile dosari katika uhakiki wa mfumo wa IFMIS, dosari katika taarifa za fedha kwenye mfumo, dosari za kiusalama katika kanzidata ya IFMIS, dosari katika utawala wa TEHAMA, dosari katika miundombinu ya Mawasiliano n.k.

Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

1.6.1 Kutokutumia mfumo wa IFMIS katika hesabu za mapato ya Hazina

Ukaguzi umebaini kwamba Mapato ya Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hayajaunganishwa moja kwa moja katika Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Serikali - IFMIS ambapo mapato hayo yaliyokusanywa huingizwa katika mfumo wa IFMIS kwa njia ya kawaida (manually). Hali hii inasababisha Serikali kukosa kupata taarifa sahihi za mapato halisi yaliyokusanywa. Hivyo, mfumo wa IFMIS unarikodi moja kwa moja upande wa matumizi tu kutoka Hazina, kwa maana ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Aidha, baadhi ya hesabu za benki zinazofanya matumizi ya Hazina hazijaunganishwa na mfumo huo kama vile hesabu ya matumizi ya miundombinu na hesabu ya matumizi ya fedha za kigeni. Hali hii imepelekea kuwepo kwa matumizi yasiyo taslim (Dummy) katika mfumo wa IFMIS.

Baadhi ya hesabu za Hazina ambazo hazijaunganishwa katika mfumo wa IFMIS ni kama zifuatazo:-

- Hesabu ya Mapato ya kitengo cha Hazina (Exchequer Revenue Account).
- Hesabu ya mapato na Matumizi ya Fedha za Kigeni (Forex Account).
- Hesabu ya Malipo ya Mikopo (Sinking Fund Account).

- Hesabu ya makusanyo yanayotokana na malipo ya VISA (CRDB Account - VISA Collections).

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa hesabu zote za mapato za Hazina zinaunganishwa na Mfumo wa IFMIS moja kwa moja badala ya kuingiza mapato hayo kwa njia ya kawaida (manually) ili kuweza kupunguza uwezekano wa kufanya makosa katika uingizaji wa mapato hayo na kuweza kudhibiti upotevu wa fedha za Umma.

1.6.2 Kutokurikiwa katika Mfumo wa IFMIS kwa fedha zinazotoka Hazina kwenda kwenye hesabu ya maendeleo kwa ajili ya matumizi ya Mfuko wa Miundombinu (Manual transfer) shilingi 67,965,543,856.71

Ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya fedha ambazo hupokewa katika Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo kutoka Hazina na baadae huhaulishwa kwenda katika Hesabu ya Mfuko wa Miundombinu iliyopo Hazina kwa ajili ya kutekeleza matumizi ya maendeleo kwa miradi mbalimbali iliyoidhinishwa na Tume ya Mipango na kulipwa kupitia hesabu ya Mfuko wa Miundombinu.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa fedha hizi hazirikodiwi katika mfumo wa IFMIS, si wakati fedha zinapokelewa katika hesabu ya matumizi ya maendeleo wala wakati zinapohaulishwa kwenda katika hesabu ya mfuko wa miundombinu.

Kiasi kilichopokelewa kutoka hazina kinaonekana tu katika taarifa ya benki (bank statement) lakini hakionekani katika daftari la fedha taslim la IFMIS (IFMIS Cash book).

Aidha fedha hizi hazionyeshwi katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki ya mwezi. Kinachofanyika ni kwamba wakati matumizi yanapofanywa katika hesabu ya mfuko wa miundombinu, fedha za mapato na matumizi yasiyo taslimu 'dummy' huingizwa katika mfumo wa IFMS ili kuathiri bajeti ya Fungu Kuu la bajeti husika.

Jadweli lifuatalo linaonyesha fedha zilipokelewa katika Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo kutoka Hazina katika kipindi cha miaka mitatu (2018/2019 – 2020/2021) ambazo hazijarekodiwa katika mfumo wa IFMIS:-

Jadweli Nambari 1: Baadhi ya fedha ambazo zimetoka Hazina kwenda Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo ambazo hazijarekodiwa katika Mfumo.

Mwaka wa Fedha	Mwezi	Kiasi Kilichoingizwa (Shs.)
2018/2019	July, 2018	2,047,434,150.00
	Aug, 2018	2,641,291,401.98
	Sep, 2018	0
	Oct, 2018	3,038,624,751.00
	Nov, 2018	2,657,211,804.00
	Dec, 2018	0
	Jan, 2019	6,184,603,612.63
	Feb, 2019	4,383,519,466.00
	Mar, 2019	5,736,578,228.10
	Apr, 2019	2,594,700,790.00
	May, 2019	2,840,842,252.00
	June, 2019	192,003,200.00
	Jumla Ndogo	32,316,809,655.71
2019/2020	July, 2019	1,787,418,524.00
	Aug, 2019	4,836,538,083.00
	Sep, 2019	2,695,520,201.00
	Oct, 2019	3,167,794,128.00
	Nov, 2019	4,804,793,562.00
	Dec, 2019	0.00
	Jan, 2020	0.00
	Feb, 2020	3,040,402,741.00
	Mar, 2020	0.00
	Apr, 2020	2,761,960,638.00
	May, 2020	2,039,839,832.00
	June, 2020	1,332,154,552.00
	Jumla Ndogo	26,466,422,261.00
2020/2021	July, 2020	1,818,768,613.00
	Aug, 2020	0.00
	Sep, 2020	2,324,184,896.00
	Oct, 2020	2,591,796,956.00
	Nov, 2020	2,447,561,475.00
	Dec, 2020	0.00
	Jumla Ndogo	9,182,311,940.00
JUMLA KUU	67,965,543,856.71	

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa hesabu zote za matumizi za Hazina ziwe zinaunganishwa na mfumo wa IFMIS ili kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha za umma na kupunguza fedha za mapato na matumizi yasiyo taslimu (dummy).

1.6.3 Dosari za taarifa za Usuluhishi wa kibenki kwa hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika uandaaji wa taarifa za usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation statements) kwa Hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo (Central Payment Office – CPO) ambazo huandaliwa kila mwisho wa mwezi.

Mapato na matumizi yasiyo taslimu (Dummy Transactions) hayaonyeshwi katika taarifa za usuluhishi wa benki ingawa yanaonekana katika daftari la mapato na matumizi la IFMIS.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba taarifa za usuluhishi wa kibenki za hesabu ya Maendeleo hazionyeshi fedha zilizopokelewa benki kutoka Hazina, fedha ambazo mwishowe huhamishiwa katika hesabu ya Miundombinu. Upokeaji wa fedha kutoka Hazina na uhaulishaji wa fedha kwenda hesabu ya miundombinu hauonyeshwi kabisa katika daftari la fedha taslim (cash book) wala katika taarifa za usuluhishiwa kibenki.

Ukaguzi umebaini kuwa kuna baadhi ya miezi haina taarifa za usuluhishi wa kibenki zilizokubaliana na bakaa za mwezi husika na kupelekea tofauti kati ya bakaa ya fedha kwa mujibu wa daftari la fedha taslim la IFMIS na bakaa ya fedha baada ya kuandaa taarifa ya usuluhishi wa kibenki. Tofauti zilizobainika ni kama ilivyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

Jadweli Nambari 2: Tofauti zilizobainika katika taarifa za usuluhishi wa kibenki za hesabu za Ofisi kuu ya malipo

Hesabu	Tarehe	Bakaa ya Fedha kwa mujibu wa Daftari la Fedha Taslim la IFMS (Shs.)	Bakaa ya Fedha kwa mujibu wa taarifa ya Usuluhishi wa kibenki (Shs.)	Tofauti (Shs.)
Hesabu ya Matumizi ya Kawaida -9928182004	31 Julai, 2018	8,847,484,357 DR	8,814,533,625 DR	32,950,732DR
Hesabu ya Matumizi ya Kawaida -9928182004	31 Disemba, 2018	21,016,848,452DR	20,775,392,142 DR	241,456,309 DR

Hesabu ya Public Debt – 9928182104	31 Januari, 2019	12,062,978,741 DR	12,737,950,875 DR	674,972,134 CR
Hesabu ya Matumizi ya Kawaida -9928182004	28 Februari, 2019	28,724,925,190 DR	28,721,636,601 DR	3,288,589 DR

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara kuhakikisha wanaondoshamapato na matumizi yasiyo taslimu (dummy) ndani ya mfumo kwa kuiwezesha kila Idara kukusanya na kutumia fedha za Serikali ndani ya Mfumo. Aidha fedha zote zinazolingia na kutoka katika hesabu za benki za serikali lazima ziwe zinahusishwa katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki za kila mwezi.

1.6.4 Tofauti kati ya fedha iliyoidhinishwa kupelekwa katika mafungu makuu ya bajeti na fedha halisi zilizohaulishwa kwenda katika mafungu hayo shilingi 1,358,829,378

Fedha kutoka Hazina hupelekwa katika Mafungu Makuu ya bajeti kupitia mfumo wa IFMIS kila mwezi kulingana na mtiririko wa fedha ulioidhinishwa kwa Wizara husika kwa kila mwezi. Fedha hizo kutoka Hazina zinaingizwa katika mfumo wa IFMIS baada ya kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa hali ya kifedha na kiuchumi.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tofauti kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali na kiasi halisi cha fedha kilichoingizwa katika Mafungu Makuu ya bajeti. Vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa tofauti hiyo havikupatikana kwa ukaguzi.

Uwepo wa tofauti kwa fedha zinazolingizwa katika Mafungu Makuu ya bajeti kama ilivyoainishwa hapo chini kunapelekea kukosekana kwa uhalali wa fedha za ziada zilizolingizwa katika Mafungu Makuu ya Bajeti. Tofauti ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadwali hapo chini:-

Jadweli Nambari 3: Tofauti kati ya fedha zilizoidhinishwa kupelekwa katika mafungu makuu ya bajeti na fedha halisi zilizohaulishwa.

Tarehe	Fedha Iliyoidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali Shs.	Fedha Halisi Iliyoingizwa katika Mfumo wa IFMIS Shs.	Tofauti Shs.
21-Dec-2016	2,507,130,644.00	3,584,112,952.00	1,076,982,308.00
6-Aug-19	5,022,325,240.00	5,036,812,740.00	14,487,500.00
11-Nov-19	6,564,238,952.00	6,589,160,452.00	24,921,500.00
25-Mar-20	55,000,000.00	250,075,070.00	195,075,070.00
23-Jun-20	9,474,456,000.00	9,521,819,000.00	47,363,000.00
Jumla			1,358,829,378.00

Ukaguzi unapendekeza kuwepo kwa mfumo wa uwazi kwa fedha zinazoidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoka hazina kwenda katika Mafungu Makuu ya bajeti ili tofauti baina ya fedha hizo iweze kubainika na kupatiwa maelezo ya wazi.

1.6.5 Fedha zilizohaulishwa mwishoni mwa mwaka wa fedha kwenda katika hesabu za Amana shilingi 5,047,449,249.16

Kwa mujibu wa kifungu nambari 52 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016, bakaa ya fedha za matumizi ambayo hayakutumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha ambao matumizi hayo yameidhinishwa itaondoshwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali au katika hesabu ya Serikali ya Mtaa kwa kadri itakavyohitajika.

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa uhaulishaji wa fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha kwenda katika hesabu za Amana kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa fedha uliokwisha malizika ambapo ruhusa ya kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali haikupatikana kwa ukaguzi. Taarifa za uhaulishaji huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 4: Fedha zilizohaulishwa mwishoni mwa mwaka wa fedha kwenda katika hesabu za Amana

Tarehe	Fedha kutoka Hesabu ya:	Fedha kwenda Hesabu ya Amana:	Kiasi cha Fedha Shs.	Fungu Kuu la Bajeti	Kumbukumbu ya Benki
29-Juni-2020	CAPITAL ACCOUNT	021103000778 KATIBU MKUU WIZARA YA KILIMO	1,300,000,000.00	WIZARA YA KILIMO	L01PV1900001873
29-Juni-2020	CAPITAL ACCOUNT	ZANZIBAR CENTRAL MISCELLANEOUS DEPOSIT – 9928161804	257,683,229.62	WIZARA YA FEDHA	F01PV1900002259
30-Juni-2020	CAPITAL ACCOUNT	ZANZIBAR CENTRAL MISCELLANEOUS DEPOSIT – 9928161804	23,846,898.00	TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA	C04PV1900000470
26-Juni-2019	CAPITAL ACCOUNT	C Miscellaneous Deposit Account	419,817,500.00	WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI	S01PV1800001282
30-Juni-2020	PUBLIC DEBT ACCOUNT	021103000709 PUBLIC DEBT DEPOSIT ACCOUNT	1,072,142,934.98	HUDUMA ZA MFUKO MKUU	F02PV1900002453
29-Juni-2020	RECURRENT ACCOUNT	ZANZIBAR CENTRAL MISCELLANEOUS DEPOSIT – 9928161804	516,706,745.56	WIZARA YA FEDHA	F01PV1900002260
27-Juni-19	RECURRENT ACCOUNT	C Miscellaneous Deposit Account	534,197,102.00	WIZARA YA FEDHA	F01PV1800002188
26-Juni-19	RECURRENT ACCOUNT	C Miscellaneous Deposit Account	923,054,839.00	WIZARA YA FEDHA	P01PV1800001483
Jumla			5,047,449,249.16		

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa kifungu nambari 52 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 kinawajibishwa kwa bakaa ya fedha za matumizi mwisho wa mwaka na kama kuna dhima ya matumizi basi taasisi ya matumizi lazima ipate ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ya kubakisha fedha hizo katika hesabu ya Amana.

1.6.6 Matumizi ya nambari moja ya kumbukumbu ya Hati ya Exchequer ya IFMIS (same reference number) kwa fedha zilizotolewa kwa Mafungu Makuu tofauti ya Bajeti.

Ukaguzi umebaini kuwa hati za utoaji fedha za Exchequer zilizomo ndani ya Mfumo wa IFMIS zinatumia nambari za kumbukumbu zinazofanana kwa fedha zilizotolewa kwenda Mafungu Makuu tofauti ya Bajeti kwa tarehe husika.

Hii inapelekea ugumu katika usawazishaji wa matumizi ya fedha za Mafungu Makuu ya Bajeti katika taarifa za upatanishi wa benki hasa kwa fedha za mapato na matumizi yasiyo taslimu (dummy) kutokana na ukweli kwamba ili matumizi ya 'Dummy' ya Fungu Kuu fulani la Bajeti yaonekane katika mfumo IFMIS ni lazima fedha zote za 'Dummy' za Mafungu Makuu mengine yenye nambari ya kumbukumbu inayofanana nayo yawe yameshasawazisha matumizi ya Fedha hizo katika mfumo.

Baadhi ya nambari za kumbukumbu zinazofanana za hati za utoaji wa fedha za Exchequer kwa vifungu tofauti vya bajeti zilizobainika ni kama inavyoonekana katika

Kiambatisho Nambari 1.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa nambari za kumbukumbu za hati za utoaji wa fedha za Exchequer kwa vifungu tofauti vya bajeti ziwe tofauti kwa kila Fungu Kuu la bajeti ili kuondosha utata wakati wa ukaguzi wa fedha hizo pamoja na kurahisisha utayarishaji wa taarifa za upatanishi wa kibenki.

1.6.7 Dosari zilizobainika katika uhakiki wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha - IFMIS.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imeanzisha mfumo wa Usimamizi wa Fedha – IFMIS kwa ajili ya kuimairisha malengo yake ya utoaji wa huduma za taarifa za fedha katika Taasisi za Serikali.

Mfumo huo umetengenezwa ili kuweka Usimamizi wa taarifa za fedha za taasisi za Serikali ambapo umegawika katika moduli tofauti ikiwemo moduli ya "Account Payable", "Account Receivable", "Purchasing Order", "Fixed Assets", "General Ledger", "Cash Management" na "e-Procurement".

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika mfumo huo wa IFMIS/EPICOR Version 10.1.4. ambapo dosari hizo zinaweza kusababisha hatari katika utendaji kazi wa mfumo huo. Baadhi ya dosari zilizomo ni kama zifuatazo:-

- i. Kuwepo kwa watumiaji wa mfumo ambao waliojirudia na wenye shaka (duplicated /ambiguous users) pamoja na watumiaji wasiojulikana (unknown users) ambao wamepewa haki kubwa za matumizi ya mfumo huo (Administrative Rights) **Kiambatisho Nambari 2 (a) Kinahusika.**

- ii. Baadhi ya watumiaji wa mfumo wa IFMIS nenasiri "Domain Password" zao zimeshaisha muda, hivyo watumiaji hao huingia kwenye mazingira ya mfumo huo kupitia akaunti za watumiaji wengine (sharing of login credentials).
- iii. Baadhi ya watumiaji wa mfumo wapo likizo kwa muda mrefu lakini ndani ya mfumo wanaonekana wapo hai (active status) na akaunti zao hazijasimamishwa. **Kiambatisho Nambari 2 (a) Kinahusika.**
- iv. Tathmini ya Upimaji wa Kuwepo kwa Vihatarishi haifanyiki ndani ya Mfumo wa IFMIS ili kuweza kubaini viashiria hatarishi vilivyomo katika mfumo huo na kudhibiti visije kutokea "Vulnerability Assessment and Penetration Testing".
- v. Kutumika kwa Akaunti Asilia za wasimamizi wa Mifumo na kanzidata "Administrators Account" ambazo akaunti hizo zilipaswa kusitishwa "disabled" na badala yake kutumika kwa haki zao tu" Administrators Rights". **Kiambatisho Nambari 2 (b) Kinahusika.**

Hali hii inaweza kusababisha kupotea au kubadilishwa kwa makusudi taarifa za fedha za Taasisi katika mfumo huo na hatimae kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara kuweza kutatua dosari zote zilizopo katika mfumo huo ili kuweza kuepuka na vihatarishi vya upotevu wa taarifa na fedha za Serikali.

1.6.8 Kukosekana kwa Muunganiko wa Moja kwa Moja wa Mawasiliano baina ya Mfumo wa IFMIS na mifumo mengine ya fedha ya taasisi za Serikali

Serikali imetengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – IFMIS ambao madhumuni yake ni kuhifadhi na kudhibiti taarifa za mapato na matumizi ya fedha za Serikali kuanzia hatua ya utayarishaji wa bajeti, utekelezaji wa bajeti na utoaji wa ripoti za bajeti katika Mawizara, Idara na Wakala katika sekta za umma.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa IFMIS haujaunganishwa moja kwa moja na mifumo mengine ya fedha ya Serikali kama vile Mifumo ya Kukusanyia Mapato na Kodi (ZRB,TRA) , Mifumo ya Kibenki (PBZ) pamoja na mifumo ya taasisi nyengine za wakala wa Serikali ambapo mifumo hiyo kwa pamoja ingeweza kuwasiliana na kupelekea taarifa za mapato kuingia moja kwa moja na kwa wakati ndani ya mfumo wa IFMIS (automatically) ili kudhibiti makosa katika usahihi wa kuingiza taarifa hizo kwa mkono na kusababisha upotevu wa mapato na matumizi ya fedha.

Kukosekana kwa muingiliano wa moja kwa moja baina ya mifumo ya fedha ya Serikali (IFMIS, ZRB, TRA, PBZ n.k) kunaweza kupelekea kufanyika kwa makosa katika uingizaji wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha za serikali na hatimae kutokea kwa upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kufanya mchakato wa kuunganisha mifumo hiyo mikuu ya fedha moja kwa moja ili kuweza kupata usahihi wa taarifa za fedha na kudhibiti upotevu wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali.

1.6.9 Kukosekana kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa "Lack of BCP & DRP".

Lengo la kuwa na Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa katika Taasisi ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti mzuri wa upatikanaji wa taarifa na kuendelea kutoa huduma bora za biashara wakati janga lolote litakapotokea katika Idara au miundombinu ya Idara.

Moja ya njia nzuri ya kuzilinda taarifa na kuendeleza Mpango wa Uendelezaji wa Biashara wakati janga litakapotokea kwenye Idara ni kuwa na mpango maalum na miundombinu madhubuti ya kuhifadhi taarifa katika sehemu iliyotengwa (offsite backup) nje ya Idara kuu.

Mpango mzuri wa Muendelezo wa Biashara ni ule ambao mara zote unakuwa imara katika usafirishaji wa taarifa kutoka sehemu kuu ya taarifa (Datacenter) kwenda sehemu nyengine ya kuhifadhi taarifa ambayo ina umbali wa masafa (offsite backup). Taarifa hizo zinasafirishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine kupitia mtandao ulio salama.

Taarifa hizo zinapohifadhiwa katika sehemu ya pili (Offsite – Backup Location) zinatakiwa zichunguzwe na kujaribiwa kwa kushirikishwa uongozi wa Idara ili kuweza kuona na kuhakikisha kwamba taarifa hizo ziko sahihi na zinaweza kupatikana wakati zitakapohitajika.

(a) Kasoro zilizobainika katika sehemu ya pili ya kuhifadhi taarifa (Disaster Recovery Site)

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu inayo sehemu ya pili (Disaster Recovery Site) iliyopo nje ya mji kwa ajili ya kuhifadhi taarifa wakati janga likitokea katika sehemu kuu ya kuhifadhi taarifa iliyopo Vuga Mjini.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba taarifa zilizohifadhiwa sehemu ya pili hazifanyiwi majaribio yoyote ya kuzichunguza ili kuhakikisha kwamba ziko vizuri na zinaweza kufanya kazi kwa usahihi wakati zitakapohitajika.

Kutofanya majaribio ya kuchunguza taarifa zinazohifadhiwa katika sehemu ya pili kunaweza kusababisha hatari ya kutopatikana kwa taarifa wakati janga litakapotokea katika sehemu kuu ya kuhifadhi taarifa na hatimae kupelekea kukosekana kwa muendelezo wa huduma za fedha katika mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kuzifanyia majaribio taarifa zinazohifadhiwa katika sehemu ya Pili ili kupata uhakika wa taarifa hizo kama zinaweza kufanya kazi kwa usahihi wakati zitakapohitajika.

(b) Kukosekana kwa Nyaraka za Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Nyaraka za Mpango wa Udhhibiti wa Kupona Maafa (Lack of BCP & DRP Documentation).

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu haina nyaraka rasmi ambazo zinaonesha mpango/muongozo kamili wa Muendelezo wa Biashara na Kupona Maafa endapo maafa (majanga) yakitokea katika Idara hiyo.

Kutokuwa na nyaraka ambazo zitakazoonesha Mpango wa Muendelezo wa Huduma za Biashara na Mpango wa Kupona Maafa katika Idara kunaweza kusababisha hasara ya kuharibika kwa vitendea kazi vya kompyuta , miundombinu ya mawasiliano na hatimae kupotea kwa taarifa muhimu katika mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi unashauri Idara kuandaa nyaraka za mpango utakaonesha muongozo kamili wa Muendelezo wa Biashara na nyaraka zenye kuonesha Mpango kamili wa kupona maafa ikiwa maafa (majanga) yatatokea katika Idara.

1.6.10 Kukosekana kwa Mkataba wa Viwango vya Utoaji wa Huduma ya Mfumo wa IFMIS baina ya Idara ya Mhasibu Mkuu na Mshauri Elekezi (Service Level Agreement – SLA).

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba Taasisi inatakiwa kufunga mkataba rasmi uliosainiwa baina ya pande mbili (Mtoaji Huduma na Taasisi itakayopewa huduma) ambapo mkataba huo utaonesha aina gani ya huduma itakayotolewa na kiwango gani cha huduma kitatolewa na "Service Provider" ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu inatumia mfumo wa usimamizi wa fedha – IFMIS ambao umetengenezwa na Kampuni ya Soft Tech Consultant Limited (STCL). Hata hivyo ukaguzi umebaini kukosekana kwa mkataba rasmi uliosainiwa ambao unaoonesha kiwango gani cha huduma za Mfumo kinachotakiwa kutolewa na Kampuni ya STCL kwa ajili ya Idara ya Mhasibu Mkuu ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kukosekana kwa mkataba wa viwango vya utoaji wa huduma (SLA) za mfumo wa IFMIS kunaweza kupelekea Idara ya Mhasibu Mkuu kutofahamu kiwango halisi cha utendaji kazi wa mfumo huo na kupelekea kutoa huduma chini ya kiwango, kutopata msaada wa kiufundi kwa wakati ,kukosa matengenezo na maboresho ya mfumo na hatimae kuingia gharama za uendeshaji zisizo za lazima.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara kuhakikisha kwamba mkataba wa viwango vya utoaji wa huduma unatengenezwa rasmi na kusainiwa ili kupata msaada mzuri wa upatikanaji wa huduma kutoka kwa kampuni ya STCL.

1.6.11 Dosari zilizobainika katika Kudhibiti matumizi ya Programu za Kompyuta na Media.

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba Taasisi ambazo zinatumia mifumo muhimu ya TEHAMA zinatakiwa kuweka udhibiti na usalama mkubwa wa taarifa ambazo zitahifadhiwa ndani ya mifumo hiyo.

Moja kati ya njia imara za kudhibiti na kuweka usalama wa taarifa za kwenye mifumo ni kuweka sera zilizobora katika matumizi ya kompyuta za ofisi pamoja na sera za matumizi ya programu (software) zinazotumika katika kompyuta hizo.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya kompyuta za Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS zina dosari mbali mbali za kiusalama ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa taarifa zilizohifadhiwa ndani yake na kupelekea kutokea kwa hatari ya kushambuliwa kwa mfumo mzima wa usimamizi wa fedha IFMIS. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Utumiaji wa " Antivirus " zilizokuwa huru na hazina leseni za matumizi.
Kiambatisho Nambari 2 (e) Kinahusika.
- b) Utumiaji wa programu za mfumo wa uendeshaji wa Kompyuta na Seva (Operating Systems) ambazo hazina leseni za matumizi na nyengine zimeshapitwa na wakati (Windows 7). **Viambatisho Nambari 2(c) na 2(f) vinahusika.**
- c) Kutodhibitiwa kwa sehemu za mawasiliano katika kompyuta kama vile sehemu za kuingiza flash, sehemu za kuingiza wire za simu, pamoja na milango ya CD/DVD. Sehemu hizi zinaweza kusababisha uingizaji wa virusi kwenye kompyuta na seva za ofisi zikiwa hazitakuwa na udhibiti mzuri.
- d) Utumiaji wa programu za "Microsoft Office" ambazo ni feki na hazina leseni za matumizi.

Kutoweka udhibiti mzuri katika matumizi ya kompyuta na media kunaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa muhimu za Idara na kuplekea kuharibika kwa mfumo wa usimamizi wa fedha.

Ukaguzi unashauri Idara kuweka udhibiti imara katika matumizi ya kompyuta pamoja na milango ya media ili kuweza kulinda taarifa za zilizomo ndani ya kompyuta na mfumo wa usimamizi wa fedha. Baadhi ya njia imara za kudhibiti upotevu wa taarifa katika kompyuta ni kama zifuatazo:-

- Kuweka sera imara za matumizi ya kompyuta katika ofisi.
- Kuweka sera imara za kudhibiti matumizi ya media kwenye kompyuta kama vile matumizi ya flash disk, CD/DVD na kuunganisha simu katika kompyuta.
- Kutumia mfumo wa network za ndani (Files and Folders Sharing - LAN) kwa ajili ya kuhamisha taarifa kutoka kompyuta moja kwenda nyengine ndani ya ofisi.

Vile vile kutumia baruapepe (emails) rasmi za ofisi kwa ajili ya mawasiliano na kusafirisha taarifa nje na ndani ya ofisi ili kuweza kudhibiti upotevu na uharibikaji wa taarifa na mfumo wa fedha wa Idara.

- Kununua programu halisi (Original and Genuine Software) zenye ubora na za kisasa ili kuweza kupata usalama "Updates" na leseni za matumizi halali ya programu hizo kwa ajili ya Ofisi. Programu halisi za kununua ili kupata usalama wa kutosha na leseni za matumizi halali zikiwemo "Windows Operating Systems, Computer Antiviruses" pamoja na "Office Packages".

1.6.12 Dosari za kiusalama katika Kituo Kikuu cha Taarifa (Datacenter) kilichopo Vuga

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali za kiusalama katika Kituo Kikuu cha kuhifadhi na kusambaza Taarifa (Dacenter) kilichopo katika Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS Vuga Mjini.

Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Idara ina Kamera za CCTV kwa ajili ya kusimamia shughuli zinazofanyika katika chumba cha Seva. Hata hivyo, ujazo wa vifaa vya kurikodia matukio (NVR - Hardisk) ni mdogo ambao ni 8TB ukilinganisha na idadi ya kamera 36 zilizopo katika jengo hilo, hii inamaanisha kwamba vifaa vya kuhifadhi matukio havitakuwa na uwezo mzuri wa kuhifadhi taarifa kwa muda mrefu.
- Mfumo wa uzimaji wa moto ndani ya kituo hicho cha taarifa haufanyi kazi. Hali hii inaweza kusababisha hatari na hasara kubwa endapo ikitokea khitilafu zozote za moto.
- Kukosekana kwa kitabu cha kumbukumbu ambacho kinatumika kwa mahudhurio ya watu wanaoingia katika chumba cha Seva.
- Kukosekana kwa mkusanyiko wa seva za mfumo ambazo ziloungwa na kufanya kazi kwa pamoja (clustering & load balancing) ili kuweza kupunguza mzigo wa kufanya kazi kwa seva moja na kuondoa tatizo za upole upole (slowness) na kuongeza uhakika wa kupata huduma.
- Seva ya uzalishaji inatumia teknolojia ya " Virtualization – Type 1 Hypervisor " ambapo toleo lake la mfumo wa uendeshaji (Operating System) ni la zamani " ESXi vCenter Server 5.5 " ambapo toleo hili kwa sasa halipati huduma kamili za kiusalama (security updates) kutoka kwa Muuzaji wa mfumo huu (Vendor).
- Kukosekana kwa ripoti za kufanya " backup " ambazo zitaonesha muda gani backup imeanza na muda gani imemaliza na muhusika alofanya uo mchakato na nani alothibitisha kama backup hiyo ipo kamili na inafanya kazi.
- Kukosekana kwa ripoti zitakazoonesha uwezo wa utendaji kazi wa wafanyakazi

wa kitengo cha TEHAMA (performance reports) ambazo zitaweza kusaidia kuelewa uwezo wa utendaji wao wa kazi na usimamizi wa mfumo wa IFMIS.

Dosari za kiusalama zilizotajwa hapo juu zinaweza kusababisha upotevu wa taarifa za fedha katika mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi unashauri Idara kuongeza usalama kwa ujumla katika Kituo Kikuu cha Taarifa kwani sehemu hiyo ni muhimu sana na kwa vile taarifa zote za mfumo wa usimamizi wa fedha zimehifadhiwa hapo.

1.6.13 Kutokuwepo na mipangilio imara ya kiusalama katika vifaa vya kuchuja mawasiliano (Firewalls) ya Mtandao.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imefunga vifaa maalum (Sophos Firewall) kwa ajili ya kuchuja taarifa zinazolingia na kutoka kwenye mtandao wa Idara kwa lengo la kudhibiti matumizi ya mtandao na kuepuka uhalifu wa mitandao kutokea katika Idara.

Ukaguzi umebaini Idara haijaweka sera na mipangilio imara katika vifaa hivyo vya kuchuja mawasiliano ili kuweza kudhibiti matumizi yasiyo salama ya mtandao wa "Internet".

Matumizi yasiyo salama ya internet ni kama vile kuweza kufungua tovuti ambazo haziko salama na zina vihatarishi vikubwa katika kusambaza virusi na kupenya kwa wahalifu wa mitandao. Baadhi ya tovuti hizo ikiwemo tovuti za kupakua, tovuti za kubeti, tovuti za mambo yanayaoenda kinyume na maadili, baadhi ya mitandao ya kijamii n.k. **Kiambatisho Nambari 2(d) Kinahusika.**

Kutokuwepo sera imara za usalama kwenye vifaa vya kuchuja taarifa za mawasiliano kunaweza kupelekea hatari ya kuingia virusi katika kompyuta na Seva zenye mfumo wa IFMIS kupitia mtandao wa Internet na vile vile kuweza kufanyika kwa mashambulizi ya mfumo huo kwa wahalifu wa mitandao.

Ukaguzi unashauri Idara iweke sera madhubuti za usalama katika vifaa vyake vya kuchujia mawasiliano ili kuweza kudhibiti matumizi ya mtandao yasiyosalama na kujilinda dhidi ya uhalifu wa mitandao pamoja na virusi.

1.6.14 Kasoro zilizobainika katika Sera za Usalama wa Matumizi ya Vifaa vya TEHAMA na Mfumo wa IFMIS (ICT Security Policy).

Sera za Usalama katika matumizi ya vifaa vya TEHAMA na Mifumo ni nyaraka ambazo ndani yake zimekusanya miongozo inayoonesha matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA na mifumo, pamoja na sheria za matumizi hayo na adhabu zinazoweza kutolewa kutokana na ukiukwaji wa sheria hizo. Sera hizo zinapoandaliwa zinatakiwa zizingatie vihatarishi vyote ambavyo vinavyoweza kutokea wakati wa utumiaji wa vifaa hivyo pamoja na mifumo ya TEHAMA kwa wafanyakazi.

Aidha, Nyaraka hizo zitatakiwa kusainiwa na uongozi kwa ajili ya kupata idhini ya matumizi na zinatakiwa zitolewe nakala na kupewa wafanyakazi wa Idara wanaotumia vifaa hivyo na mifumo ambapo wafanyakazi hao baadae watahitajika kupata mafunzo yenye kuleta ufanisi na weledi juu ya matumizi sahihi na salama ya vifaa hivyo pamoja na mifumo na hatimae kuvitunza na kuviweka katika hali ya usalama.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba nyaraka za Sera za Usalama za Idara ya Mhasibu Mkuu zilizoandaliwa kwa matumizi ya TEHAMA zina mapungufu ikiwa ni pamoja na kutokufanyiwa mafunzo kwa wafanyakazi ili kupata uelewa wa matumizi salama ya vifaa vya TEHAMA pamoja na Mifumo yake.

Kutofanyika kwa mafunzo ya sera za usalama wa matumizi ya Vifaa vya TEHAMA kwa wafanyakazi kunaweza kupelekea kufanyika kwa matumizi mabaya ya vifaa pamoja na mifumo na badae kusababisha upotevu na kuleta vihatarishi katika taarifa za Ofisi na rasilimali zake.

Ukaguzi unashauri Idara ya Mhasibu Mkuu kuimarisha taarifa zilizomo ndani ya nyaraka za sera ya Usalama wa matumizi ya vifaa vya TEHAMA pamoja na mifumo yake na kutoa mafunzo kwa wahusika ili kuweza kutumika vifaa hivyo kwa uweledi na ufanisi na kupelekea kupunguza hatari za upotevu wa taarifa na uharibifu wa vifaa.

1.6.15 Kutofanyika kwa Upimaji wa Mazingira Hatarishi na Jaribio la Upenyaji katika Mtandao (Vulnerability Assessment and Penetration Testing - VAPT).

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba Taasisi inatakiwa kufanya zoezi la upimaji wa Mazingira Hatarishi na Jaribio la Kupenya kwenye mtandao ili kupata taarifa. Lengo la kufanya zoezi hilo ni kuweza kuangalia viashiria hatarishi vyote ambavyo vipo au vinavyoweza kutokea katika mtandao wa Idara na kuziba maeneo yote yaliyo hatari ili kuweza kuongeza usalama katika mtandao kwa kudhibiti vyanzo vyote hatarishi.

Aidha zoezi hilo la upimaji wa mazingira hatarishi pamoja na jaribio la kupenya kwenye mtandao wa Idara kwa kawaida linafanyika angalau mara mbili kwa kila mwaka ili kuweza kujiridhisha kwamba hali ya mtandao wa Idara ni salama dhidi ya virusi na wahalifu wa mitandao.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS haijawahi kufanya zoezi hilo la upimaji wa mazingira hatarishi na jaribio la kupenya kwenye mtandao wake ili kuweza kuona maeneo gani yaliyo na vihatarishi vya kupatikana kwa taarifa.

Hivyo basi Idara haiwezi kujua ni sehemu gani katika mtandao wake na miundombinu yake ya mawasiliano inaweza kuwa dhaifu na kusababisha vihatarishi na kuweza kudhibiti sehemu hizo.

Kutokufanya zoezi hilo kunaweza kusababisha taarifa za kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – IFMIS kuingiliwa na wahalifu wa mitandao na kuweza kubadilishwa kwa taarifa za fedha za taasisi mbali mbali na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za Serikali pamoja na uharibifu wa taarifa za fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara kufanya zoezi la upimaji wa mazingira hatarishi na jaribio la kupenya kwenye mtandao wa Idara kupitia miundombinu ya Idara ili kuweza kudhibiti maeneo yote hatarishi katika mtandao huo.

1.6.16 Kukosekana kwa Nyaraka za Haki za Watumiaji wa Mfumo wa IFMIS.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu imeunganisha watumiaji mbali mbali wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – IFMIS lakini Idara haina nyaraka ambazo zinaonesha mipaka ya haki za watumiaji hao wa Mfumo wa IFMIS. Aidha ukaguzi umebaini kwamba hakuna mapitio yoyote ya mara kwa mara ya kuchunguza mipaka ya haki za watumiaji wa mfumo huo.

Ukaguzi ulipata taarifa kutoka kwa Msimamizi wa Mfumo wa IFMIS kwamba uhakiki wa mwisho uliofanyika kuangalia watumiaji wa mifumo ulifanyika mwezi wa Disemba 2020, lakini hakuna nyaraka rasmi zozote zilizotengenezwa kuhusiana na uhakiki huo.

Kukosekana kwa nyaraka za uhakiki wa haki za watumiaji wa mfumo wa IFMIS na kutofanya uhakiki wa mara kwa mara wa haki za watumiaji wa mfumo wa IFMIS kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya mfumo na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri kwamba Idara iandae nyaraka za haki za watumiaji wa mifumo na kuzipitia nyaraka izo mara kwa mara ili kudhibiti utumiaji mabaya wa mfumo wa IFMIS.

1.6.17 Kukosekana kwa Mpango Mkakati wa TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS haijaandaa Mpango Mkakati wa Tehama ambao ungeweza kusaidia Idara kufanikisha malengo yake kwa ufanisi zaidi kupitia TEHAMA.

Kutokuwepo kwa Mpango Mkakati wa TEHAMA katika Idara kunaweza kusababisha malengo ya TEHAMA kutokwenda sambamba na malengo ya Idara na kufanyika maamuzi ya TEHAMA yasiyokuwa na tija ambayo yanaweza kupelekea kupungua kwa kasi ya maendeleo ya utoaji wa huduma ya Mfumo wa IFMIS kwa Idara na hatimae kusababisha upotevu wa taarifa za fedha.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kuandaa Mpango Mkakati ili kufanya malengo yake yaende sambamba na malengo ya Idara na kupelekea kupatikana kwa huduma bora ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha.

1.6.18 Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya Mifumo ya TEHAMA

Utaratibu uliobora (Best Practise) unaeleza kwamba Mkuu wa Idara atapaswa kuunda Kamati Tendaji ambayo itakuwa na lengo la kushughulikia masuala yote ya maendeleo ya utendaji wa TEHAMA, maendeleo ya utoaji wa huduma za TEHAMA na maamuzi yake katika Idara pamoja na kuhakikisha sera na mikakati yote ya TEHAMA katika Idara inasimamiwa na kutekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha wajumbe wa Kamati hiyo wanatakiwa kupewa Hadidu Rejea na kutengeneza Hati za uendeshaji wa vikao vya TEHAMA.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS haina Kamati Tendaji ya TEHAMA ili kuweza kusaidia utekelezaji wa malengo na mikakati ya TEHAMA katika Idara.

Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA katika Idara ya Mhasibu Mkuu kunaweza kusababisha mipango ya TEHAMA kutotekelezwa ipasavyo na kupelekea kutofanikisha malengo kwa ufanisi katika Idara.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara kuunda Kamati Tendaji ya TEHAMA ili kuandaa mipango mizuri ambayo italeti maendeleo katika utoaji wa huduma za TEHAMA na kupelekea kufanyika kwa maamuzi yenye tija katika Idara.

Aidha kuwepo kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA kutaweza kuhakikisha sera, na mikakati yote ya TEHAMA katika Idara inasimamiwa na kutekelezwa kwa ufanisi.

1.6.19 Kukosekana kwa Mafunzo ya Usalama wa Mfumo wa IFMIS kwa Wafanyakazi wanaosimamia Mfumo wa IFMIS katika Idara ya Mhasibu Mkuu.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa Idara ya Mhasibu Mkuu wanaosimamia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (Technical Support & Application) kwa muda mrefu hawajapatiwa mafunzo maalum ya Usalama wa Mfumo Usimamizi wa Fedha (IFMIS Security Awareness Training Program). Aidha ukaguzi umebaini mara ya mwisho kupata mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi hao ni mwaka 2018 ambapo hadi sasa kuna mabadiliko mengi yamefanyika katika Mfumo lakini hakuna mafunzo kamili yaliyofanyika kuhusiana na mabadiliko hayo.

Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara ya Usalama, Usimamizi na Uendeshaji wa mfumo wa IFMIS kunaweza kusababisha kukosekana kwa usimamizi mzuri wa utumiaji wa mfumo na hatimae Idara kuingia gharama za uendeshaji wa mfumo zisizo na ulazima.

Ukaguzi unashauri Idara kuwafanyia mafunzo ya mara kwa mara ya usalama wa mfumo kwa wafanyakazi wa kitengo cha IFMIS ili kuweza kuwa kusimamia vizuri na kupata taaluma ya kisasa kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya sayansi na teknolojia. Aidha mafunzo hayo yataweza kuondosha gharama za kumwita Mshauri Elekezi mara kwa mara kuja kutatua changamoto zitakazojitokeza katika mfumo.

1.6.20 Kukosekana kwa Hati ya Muongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMIS (Lack of Updated User Manual Document - IFMIS).

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu imeingia mkataba na Kampuni ya Mshauri Elekezezi ya Soft Tech (Soft Tech Consultancy Ltd) kwa ajili ya utengenezwaji wa Mfumo wa IFMIS ambao unatumika kwa ajili ya kusimamia taarifa za matumizi ya fedha kwa Serikali.

Mfumo huo wa IFMIS ulianza rasmi kufanya kazi Julai 2015 ambapo hati ya muongozo wa matumizi (User Manual Version 1) wa 09/04/2015 uliotolewa na baadae mfumo huo kufanyiwa marekebisho mwezi wa Machi 2018.

Hata hivyo ukaguzi haukuweza kupata kwa hati ya sasa ya muongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMIS iliyotolewa rasmi kwa ajili ya toleo jipya lililofanyiwa marekebisho la Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – IFMIS.

Kukosekana kwa muongozo wa sasa wa mtumiaji wa Mfumo wa IFMIS kunaweza kusababisha watumiaji wa mfumo kutotumia vizuri mfumo hiyo na kupelekea kupotea taarifa.

Ukaguzi unashauri kwamba Idara iongeze jitihada za uwekaji wa muongozo mpya wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMS (IFMIS current user manuals documents) kutoka kwa Mshauri Elekezi ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kwa usalama kwenye mfumo huo.

1.6.21 Kukosekana kwa Msaada wa Kiufundi kwa Watumiaji wa Mfumo wa IFMIS waliopo kwenye Wizara, Idara na Mawakala (MDAs).

Moja ya majukumu ya wafanyakazi wa kitengo cha IFMIS ni kutoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo ambao wapo ndani ya Idara ya Mhasibu Mkuu na watumiaji wa mfumo ambao wanaotumia wakiwa katika Wizara, Idara na Wakala.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa kitengo cha utoaji wa msaada wa kiufundi (Technical Support Unit) hawatoi ushirikiano mzuri wa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo ambao wapo katika Mawizara, Idara nyengine na Mashirika.

Kutotoa ushirikiano mzuri wa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo walioko katika Mawizara, Taasisi na Mashirika mengine kunaweza kusababisha watumiaji wote walioko kwenye Mawizara na Taasisi kufuata huduma hiyo katika Idara ya Mhasibu Mkuu na hatimae kupelekea ucheleweshwaji wa malipo ya fedha katika Serikali.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kuandaa mpango mzuri wa kuwapa msaada wa kiufundi watumiaji ambao wapo nje ya Idara.

1.6.22 Kukosekana kwa Hati ya Muongozo wa Mpangilio wa Usalama wa Mifumo na Miundominu ya TEHAMA iliyopo katika Kitengo cha IFMIS.

Ukaguzi umeangalia kwa kina mipangilio ya kiusalama ya mfumo wa IFMIS, programu pamoja na kompyuta ambazo zimeunganishwa na mfumo huo kwa kiasi gani taarifa zinalindwa na kubaini kasoro za kiusalama katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kukosekana kwa Hati za mipangilio ya Usalama

Ukaguzi umebaini Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali haikuandaa nyaraka/hati ambazo zinaonesha mipangilio ya usalama wa mfumo pamoja na vifaa vyote vinavyotumika katika mazingira ya mfumo.

Mpangilio wa usalama wa mifumo ni Sera au nyaraka ambazo zimetengenezwa na zimehakikiwa na uongozi na zinaeleza kwa uwazi jinsi ya kuweka mipangilio iliyobora katika kuimarisha usalama wa taarifa katika mifumo na vifaa vyote vinavyotumika katika Idara hiyo.

Kutokuweka mipangilio ya usalama wa taarifa katika mifumo kunaweza kusababisha ongezeko la hatari kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo.

Ukaguzi unashauri Idara iandae nyaraka/ Sera ambayo itaonesha mpangilio mzima wa usalama wa mfumo wa IFMIS na vifaa/kompyuta zote ambazo zimeunganishwa na mfumo huo.

(b) Kukosekana kwa utaratibu wa kupitia mipangilio ya Usalama wa Taarifa.

Utaratibu uliobora (Best Practise) unaeleza kwamba Taasisi inahitaji kufanya mapitio ya mara kwa mara katika mipangilio yake yote ya kiusalama katika Seva na Kanzidata zake ili kuweza kupata uhakika wa usalama wa taarifa hizo dhidi ya wahalifu wa mitandao au wasaliti kutoka ndani ya Taasisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali haijaweka utaratibu wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mipangilio ya usalama katika Seva pamoja na kanzidata (Database) pamoja na miundombinu ya mawasiliano katika kitengo chake cha IFMIS hali inayopelekea kushindwa kutambua iwapo kama Seva, Kanzidata na miundombinu yake ipo salama.

Kutokuweka utaratibu wa mapitio ya mpangilio wa kiusalama wa taarifa pamoja na vifaa unaweza kusababisha hatari ya uvujaji na upotevu wa taarifa.

Ukaguzi unashauri Idara ya Mhasibu Mkuu kuanzisha na kufanya mapitio (kukagua) ya mara kwa mara mipangilio yake ya usalama wa mifumo na vifaa vya mtandao vilivyounyanishwa na mfumo huo ili kuweza kuongeza usalama wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na taarifa zake.

1.6.23 Kukosekana kwa Usimamizi wa Matukio ya Usalama

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS haina utaratibu na mpango mzuri wa kuonesha jinsi ya kuripoti, kuchunguza na kutatua matukio ya usalama. Hali hii imesababishwa na kukosekana kwa nyaraka/muongozo rasmi ambao utaonesha utaratibu mzima utakaotumika kusimamia matukio ya usalama.

Kutokuwa na usimamizi mzuri wa matukio ya kiusalama kunaweza kupelekea uvujaji au ubadilishwaji wa taarifa za fedha katika mfumo wa IFMIS na hupelekea upotevu na matumizi mabaya ya fedha.

Ukaguzi unashauri Idara ya Mhasibu Mkuu kuanzisha utaratibu maalum wa usimamizi wa usalama na kuthibitishwa na uongozi wa Idara ili kuongeza usalama wa taarifa zilizomo ndani ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMIS).

1.6.24 Kukosekana kwa daftari la kumbukumbu za utendaji kazi kwa Muuzaji wa Mfumo wa IFMIS.

Usimamizi wa utendaji kazi wa muuzaji wa mifumo unajumuisha ufuatiliaji na uaminifu wake katika kufanya kazi pamoja na kutoa huduma bora kwa mteja wake ambapo Muuzaji anatakiwa kutoa huduma hizo kwa usahihi na kwa wakati.

Aidha Taasisi za umma zinapaswa kutunza kumbukumbu za utendaji kazi za Muuzaji ili kuweza kusaidia kufanya maamuzi sahihi ya kuendelea nae wakati mkataba wake unapoisha wa utendaji kazi.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu – IFMIS haijatayarisha daftari la kuweka kumbukumbu za utendaji kazi wa Muuzaji wa mfumo wa IFMIS ili kuweza kuwa na kumbukumbu za utendaji kazi.

Kutoweka kumbukumbu za utendaji wa kazi wa muuzaji wa huduma (Mfumo wa IFMIS) kunaweza kupelekea kufanya maamuzi yasiyo sahihi kwa kumuongezea mkataba muuzaji ambae utendaji wake ni dhaifu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara kuanzisha daftari maalumu la kuweka kumbukumbu za utendaji kazi wa Muuzaji wa Mfumo wa IFMIS ili kuweza kupima utendaji kazi wake na kufanya maamuzi sahihi endapo mkataba wake utakapomaliza.

SURA YA PILI

2.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA BODI YA MAPATO ZANZIBAR – ZRB

2.1 UTANGULIZI

Bodi ya Mapato Zanzibar ilianzishwa kwa sheria nambari 7 ya mwaka 1996 kuwa ni Wakala mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ukusanyaji na usimamizi wa kodi zote za vyanzo vya ndani vya mapato yasiyokuwa ushuru wa forodha na Kodi ya mapato ambayo yanasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Bodi ya Mapato Zanzibar imeanza kazi kuanzia Julai, 1998.

Bodi ya Mapato Zanzibar inaendelea kutekeleza mpango wake wa muda mrefu wa kuboresha huduma zake kwa lengo la kuunganisha huduma zake ili kurahisisha kazi na kutoa taarifa na huduma bora kwa Bodi ya Mapato Zanzibar na kwa walipa kodi. Miongoni mwa hatua wa uboreshaji wa huduma za ZRB ni pamoja na utumiaji wa mifumo mbali mbali ya kielektroniki ikiwemo mfumo wa ukusanyaji wa mapato na kodi (ZITAS), Mfumo wa utendaji kazi wa Bodi (ERP), mfumo wa kiuhasibu (SAGE PASTEL) na hivi sasa ZRB inaandaa mfumo mpya wa ukusanyaji mapato uliunganishwa na mashine za EFD (VFDMS).

MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

Baadhi ya hoja zilizobainika katika ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya Bodi ya Mapato Zanzibar ni kama zifuatavyo:-

2.1.1 Dosari zilizobainika katika utengenezaji wa mashine za EFD na Mfumo wa kukusanyia Mapato wa VFDMS

Bodi ya Mapato Zanzibar ilifunga mkataba na kampuni ya Norway Registers Development AS kwa kushirikiana na Kampuni ya NRD System UAB pamoja na kampuni nyengine mbali mbali kupitia mkataba nambari ZRB/NCB/G/03/2017/2018 kwa lengo la kupata Ushauri elekezi, utengenezaji na Utumiaji wa vifaa vya Electronic Fiscal Device (EFD) ambavyo vitaunganishwa na mfumo wa Virtual Fiscal Devices Management System (VFDMS). Mkataba huo ulikuwa na thamani ya **USD 1,352,622.00** (bila ya VAT) na muda wa kumalizika kazi ni miezi kumi na nane (18).

Malengo ya kuanzishwa kwa mfumo huo yalikuwa ni kama yafuatavyo:-

- Kununua mashine za EFD na kutengeneza Mfumo wa VFDMS ambao utatumia mashine hizo.
- Kutoa huduma za kisasa na kwa wakati (real-time) kwa walipakodi wa Zanzibar pamoja na Taasisi zinazokusanya mapato yasiyokuwa ya kodi

Aidha miundombinu ya vifaa mbali mbali vya mfumo huo vimenunuliwa na kufungwa katika ofisi ya ZRB ambapo malipo ya asilimia 50 yamelipwa kwa Mshauri elekezi (Vendor) na asilimia 30 yamelipwa kwa muuzaji wa vifaa vya EFD na mtengenezaji wa mfumo huo (Software Developer).

Ukaguzi umebaini kwamba licha ya kuwa gharama za awali zimeshalipwa lakini mfumo huo wa VFDMS umesitishwa kuendelezwa na bado haujaanza kazi kutokana na kutokubaliana kwa mahitaji pamoja na vigezo vya utendaji ambavyo vimewekwa ndani ya mkataba baina ya kamati ya majaribio ya mfumo huo ya ZRB (System Acceptance Committee) pamoja na mtengenezaji wa mfumo huo wa EFD/VFDMS (System Developer).

Aidha ukaguzi umebaini dosari zifuatazo katika ufuatiliaji wa mradi huo.

- Kukosekana kwa msimamizi wa mradi (project manager) ambae angeweza kusimamia vizuri utekelezaji wa mradi huo.
- Hati ya Mchakato wa Biashara (Business Process Document) haikuandaliwa na ZRB ambayo ingeonesha mchakato (muongozo) mzima wa utendaji wa kazi na kupewa Mshauri elekezi/Mtengenezaji wa mfumo ili kutengeneza vizuri mfumo huo.
- Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA (ICT Steering Committee) ambayo ingeweza kufuatilia kwa kina na kutoa mawazo na maamuzi sahihi kuanzia hatua za awali hadi kukamilika kwa mradi huo.
- Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa fedha za Serikali kutokana na kutokufata taratibu za kusitisha mikataba ya mradi ambapo malipo ya awali yameshafanyika na kupelekea kupatikana hasara kubwa kwa Serikali.
- Kukosekana kwa mafunzo katika Idara ya TEHAMA ya usimamizi na utumiaji wa teknolojia mfumo wa VFDMS.

Kusitisha kuendelea utengenezaji wa mradi huo, kutoshirikisha kada muhimu (ICT) katika kamati ya majaribio ya mfumo pamoja na kutokuwa na kamati Tendaji ya Tehama katika Bodi ya Mapato kunaweza kepelekea kutokamilika kwa wakati malengo yaliyokusudiwa , kukosa ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo huo na hatimae kusabasisha hasara kubwa katika Serikali.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa ZRB kufanya ufuatiliaji wa kina kuhusiana na ukamilishaji wa mradi wa EFD/VFDMS na kutafuta njia sahihi ili kuweza kuendelea mfumo huo na kuweza kuepuka kuingia hasara kwa fedha za Serikali.

2.1.2 Dosari zilizobainika katika Mfumo wa Tax Block Management Information System (TBMIS)

Bodi ya Mapato Zanzibar imefunga mkataba wenye thamani ya shilingi **210,545,544.00** na Kampuni ya Rahisi Solutions Limited ikishirikiana na kampuni ya Business Connexion (T) Ltd iliyopo Zanzibar ambapo mkataba huo ulisainiwa tarehe 31/05/2019 kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo wa kuwatambua walipakodi waliopo mitaani kwa kutumia njia ya Block (Tax Block Management Information System – TBMIS).

Lengo la kuanzisha mfumo huo wa TBMIS ni kuweza kuunganisha walipakodi wote ambao wapo katika mtaa mmoja au eneo moja kwa kuwatengenezea "Block" lao la kipekee na kuingiza taarifa zao katika block hilo ili iwe rahisi kuwatambua, kuwasimamia, kuwafuatilia na kukusanya kodi zao.

Mfumo huo umeunganishwa na mfumo mwengine wa GIS (Geographical Information System) ambao unaonesha eneo (mtaa) halisi lilipo block na walipa kodi wote wanaopatikana hapo.

Ukaguzi umebaini Bodi ya Mapato kufunga mkataba mwengine wa nyongeza (Addendum No.2) uliosainiwa tarehe 05/08/2019 wenye lengo la kuongeza kipengele kipya ambacho kinaeleza kwamba Muuzaji atatengeneza vipande 10,000 vya aluminium vyenye gharama za **USD 8,600** (bila ya VAT) na kuvitia nambari ya utambuzi (code No.) kwa ajili ya kuviweka kwenye mitaa ili kupata utambuzi wa mtaa na Block zake kwenye mfumo.

Aidha ukaguzi umebaini mfumo huo tayari umetengenezwa na unatumika katika Bodi ya Mapato lakini dosari mbali mbali zimebainika katika mfumo huo kama kama zifuatazo:-

- Mfumo ulotumika wa GIS haukuweza kuunganishwa na mtandao halisi wa Google Map ili kuweza kupata taarifa sahihi za mitaa na kutoa ripoti za uhakika za walipakodi. (mfano: nearby identification locations).
- Mfumo huo wa TBMIS haujaunganishwa na Mfumo Mkuu wa ukusanyaji wa kodi (ZITAS) ili kuweza kuingizwa moja kwa moja taarifa za kodi wakati zinapokusanywa.
- Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa fedha za Serikali kutokana na Bodi ya Mapato kuingia gharama mara mbili za mikataba. Gharama za mkataba wa kwanza ni shilingi 210,545,544.00 na gharama za mkataba wa nyongeza ni USD 8,600.
- Upembuzi Yakinifu wa kina haukufanyika wakati wa utengenezaji wa mfumo huo.
- Mahitaji ya watumiaji wa mfumo huo hayakupewa kipaombele wakati wa utengenezaji wa mfumo huo, hii ni kutokana na kukosekana kwa ripoti kamili

kutoka kwa watumiaji itakayoonesha kukubalika kwa utendaji wa mfumo huo.

- Kukosekana kwa Hati za Mchakato wa Biashara (Business Process Documents) na kukosekana kwa usimamizi mzuri wa utengenezaji wa mfumo wa TBMIS ambao umepelekea Bodi ya Mapato Zanzibar kuingia gharama nyengine kwa ajili ya kufunga mkataba wa nyongeza (Addendum No. 2).
- Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA katika Bodi ya Mapato Zanzibar (ICT Steering Committee) ambayo itaweza kufanya upembuzi yakinifu na kutoa maamuzi sahihi juu ya kila hatua za utengenezwaji wa mifumo ya TEHAMA katika Bodi.
- Kukosekana kwa hati za matumizi (user manually & Technical documents) kwa wasimamizi na watumiaji wa mfumo wa TBMIS.
- Kukosekana kwa mafunzo ya kina kwa watumiaji na wasimamizi wa mfumo huo.

Kutokana na kasoro zilizotajwa hapo juu ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuchukuwa jitihada kubwa za kuweza kufuatilia na kufanya Upembuzi Yakinifu wa kina kabla ya kuanzisha miradi ya kutengeneza mifumo pamoja na kuunda kamati Tendaji ya TEHAMA iliyokuwa imara ili kuweza kuepuka hasara zinazoweza kujitokeza kutokana na gharama kubwa zitakazotumika katika utengenezaji wa mifumo ambayo haitakuwa na ufanisi na tija katika utekelezaji wake.

2.1.3 Kukosekana kwa Muunganiko wa Mawasiliano ya Moja kwa Moja baina ya Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato na Kodi (ZITAS) na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha wa Serikali (IFMIS).

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar imetengeneza Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Mapato na Kodi (ZITAS) kwa lengo la kusimamia taarifa zote za mapato na kodi zinazokusanywa na kupelekwa Serikalini kutoka kwa walipa kodi. Mfumo huo wa ZITAS kwa sasa unafanya kazi kwa miaka 7 tangu ulipoanzishwa.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa ZITAS haujaunganishwa na kuwasiliana moja kwa moja na Mfumo wa Mkuu wa Usimamizi wa Fedha wa Serikali (IFMIS) uliopo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kuweza kufanya mifumo hiyo ionane na kupelekea mapato hayo ya fedha kuonekana moja kwa moja na kwa wakati kwenye mfumo wa IFMIS.

Hadi sasa taarifa za ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka ZRB zinaingizwa katika Mfumo wa IFMIS kwa njia ya kawaida "manually".

Kukosekana kwa muingiliano wa mawasiliano baina ya mfumo wa ZITAS na mfumo wa IFMIS kunaweza kupelekea kuingizwa taarifa zisizo sahihi za mapato na kusababisha upotevu wa mapato ya fedha kwa Serikali.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar na Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kufanya mawasiliano ili kuweza kuiunganisha mifumo hiyo mikuu ya fedha kwa lengo la kupata usahihi wa taarifa za fedha na kwa wakati pamoja na kudhibiti upotevu wa fedha katika Serikali.

2.1.4 Kutofanyika kwa usafishaji wa taarifa zilizomo ndani ya Kanzidata ya Mfumo wa ZITAS. (ZITAS Database Cleaning).

Wakati wa uhakiki wa taarifa zilizomo ndani ya Kanzidata ya ZITAS (ZITAS Database) hasa katika moduli ya Walipa Kodi (Large and Small Taxpayers) ukaguzi umebaini kwamba ZRB haijawahi kufanya uhakiki wowote wa taarifa za walipa kodi zilizomo katika mfumo wa ZITAS ili kuweza kusawazisha au kuziondoa taarifa ambazo zimeharibika, taarifa zilizoingizwa kimakosa, taarifa za walipa kodi ambao wamefariki au taarifa ambazo kwa njia moja au nyengine hazihitajiki tena ndani ya mfumo huo "Gabbages" .

Tatizo hilo limesababisha baadhi ya watumiaji wa mfumo wa ZITAS kukataa kufanya kazi ndani ya mfumo huo na hatimae kufanya kazi katika programu nyengine ndogo ndogo (Microsoft Excel) kutokana na kutoziamini taarifa za mahesabu zinazozalishwa na mfumo huo.

Kutofanyika kwa usafishaji na uondoaji wa taarifa zilizokosewa au zisizohitajika ndani ya mfumo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa taarifa zisizo sahihi na kusababisha kufanyika kwa makosa katika utengenezaji wa mahesabu ya mapato, kodi pamoja na hesabu za madeni ya walipa kodi na hatimae kutokea kwa upotevu wa mapato ya Bodi.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuchukuwa jitihada za makusudi za kusafisha taarifa zilizomo ndani ya Kanzidata ya mfumo wa ZITAS ili mfumo huo uweze kufanya kazi kwa ufanisi, ubora na kuleta tija kwa Bodi ya Mapato Zanzibar.

Aidha katika kuchukuwa jitihada za usafishaji wa Kanzidata ya ZITAS ni vyema Uongozi kuunda kamati maalum ambayo itashirikisha Idara na vitengo mbali mbali ikiwemo vitengo vinavyohusika na uingizaji pamoja na utaoaji wa taarifa (Data Entries), vitengo vinavyohusika na ufuatiliaji pamoja na uangalizi wa uwepo wa walipa kodi (Enforcement), kitengo cha TEHAMA kwa ajili ya kufanya uhakiki wa taarifa zitakazobadilishwa au kutolewa katika Kanzidata ya ZITAS (verification) na vitengo vyengine vitakavyohusika na zoezi hilo.

2.1.5 Kukosekana kwa utaratibu mzuri wa uwajibikaji na ufatiliaji wa madeni ya walipa kodi waliosajiliwa na Mfumo wa ZITAS.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa ZITAS umeweza kuweka taarifa mbali mbali za Usajili wa walipa kodi wakubwa na wadogo waliopo Unguja na Pemba. Taarifa hizo za usajili ikiwemo aina ya biashara ya mlipa kodi, tarehe na mwaka wa usajili, sehemu

ya kufanyia biashara n.k.

Baada ya usajili kufanyika katika mfumo wa ZITAS , Mfanya biashara hulipa kodi kwa utaratibu ambao umepangwa na Bodi kwa mfano kulipa kodi kwa mwezi, kwa mizezi mitatu, kwa mwaka n.k. ambapo kodi hizo hulipwa kupitia nambari za usajili za TIN zilizounganishwa na mfumo wa ZITAS. Mapato yanayokusanywa hupelekwa na kuingizwa katika Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Fedha wa Serikali (IFMIS) uliopo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Hata hivyo ukaguzi umebaini Bodi ya Mapato haijaweka utaratibu mzuri wa kufanya bidii ya ufuatiliaji wa madeni ya walipa kodi ambao hawaleti mrejesho wa fedha (kodi), hivyo kusababisha wateja wengi kuendelea kutolipa kodi na wengine kulipa kodi kwa uchache.

Kutokuweka utaratibu mzuri wa kufuatilia madeni ya walipa kodi kunaweza kupelekea kupungua kwa upatikanaji wa mapato ya Bodi na kupelekea upungufu wa mapato Serikalini. Baadhi ya wateja ambao wamesajiliwa katika Mfumo wa ZITAS lakini hawajalipa kodi tangu waliposajiliwa ni kama wafuatao:-

Jadweli Nambari 5: Baadhi ya wateja ambao wamesajiliwa katika Mfumo lakni hawajawahi kulipa kodi tangu waliposajiliwa.

Namba	Nambari ya Certificate	Jina la Kampuni	Tarehe ya Kusajiliwa	Aina ya Kodi
1	Z025662649	BF COMPANY LIMITED	18/06/2020	Stamp Duty
2	Z0256529810	NEW VISION CONSORTIUM	22/06/2020	Stamp Duty
3	Z025654156	ISLAND INNOVATION COMPANY LTD	29/06/2020	VAT
4	Z025658116	ZANZIBAR SPORTS LINKAGE(SMS=PRIVATE) CO. LTD	29/07/2020	Stamp Duty
5	Z025880479	SHARUKI IT AND SECURITY COMPANY LTD	05/12/2020	Stamp Duty
6	Z0256693710	BABA THREE STORE COMPANY	11/09/2020	VAT
7	Z025672691	JUPITER COMPANT LIMITED	01/10/2020	VAT
8	Z025676354	FLAMINGO COMPANY LIMITED	06/11/2020	VAT
9	Z0256669410	PWANI HAULIERS LIMITED	22/07/2020	VAT
10	Z026664210	SERTA CO. LIMITED	18/08/2020	VAT

2.1.6 Kutoshirikishwa kwa wafanyakazi katika utengenezaji wa Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ZITAS.

Ukaguzi umebaini kwamba ZRB inaendelea kutumia mfumo wa Usimamizi wa Mapato (ZITAS) ambao umetengenezwa na Muuzaji kutoka USA Marekani tangu mwaka 2012/2013.

Hata hivyo ukaguzi umebaini wafanyakazi wanaotumia mfumo wa ZITAS hawakushirikishwa katika hatua ya awali ya utengenezaji wa mfumo huo ili kuweza kutoa maoni na mahitaji yao ya utendaji kazi katika mfumo huo, hivyo kupelekea mfumo kutofanya kazi kama ilivyotarajiwa kulingana na mahitaji ya watumiaji wa mfumo huo.

Kutokushirikisha watumiaji (wadau) kuanzia hatua ya awali ya utengenezaji wa Mfumo kunapelekea kutokezea kwa changamoto nyingi za kiutendaji ndani ya mfumo na hatimae kupelekea kutokea kwa gharama zisizo za lazima.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi kushirikisha watumiaji wa mfumo ili kuweza kuendelea kupata mahitaji muhimu katika utendaji wa mfumo wa ZITAS na kupelekea mfumo huo kufanya kazi kwa ufanisi na weledi.

2.1.7 Dosari zilizobainika katika Mfumo wa Hesabu wa SAGE PASTEL

Sage Pastel Accounting System ni mfumo wa mahesabu ambao unatumika katika Bodi ya Mapato Zanzibar kwa lengo la kusimamia taarifa za matumizi ya Bodi hiyo.

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika za kiusalama na za utendaji wa mfumo huo. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Mfumo wa Sage Pastel unashindwa kutengeneza ripoti kamili za hesabu za mwisho wa mwaka, hivyo inapelekea kutoaminika kwa ripoti zinazotolewa na mfumo huo na kusababisha wafanyakazi kutumia Microsoft Excel kwa ajili ya kutengeneza Ripoti za hesabu za mwisho wa mwaka.
- Mfumo wa Sage Pastel unaruhusu mtumiaji yoyote kuweza kubadilisha tarehe za nyuma ambapo miamala ya hesabu imefanyika bila ya kipingamizi chochote kutokea katika mfumo au kupata ruhusa kwa Uongozi.
- Mfumo wa Sage Pastel haumlazimishi mtumiaji kubadilisha nenosiri (password) kila baada ya muda maalum (siku 30 au siku 90).
- Mfumo wa Sage Pastel haujazingatia taratibu na sheria katika utengenezaji wa nenosiri (mchanganyiko wa herufi na nambari).
- Mfumo wa Sage Pastel haumfungii mtumiaji wakati anapokosea zaidi ya mara tatu kuingiza nenosiri zaidi.
- Akaunti za watumiaji hazina kikomo cha muda wa matumizi "never expired".
- Kutofanyika kwa mchakato wa uwekaji wa taarifa katika mfumo huo (backup of data).

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuamua aina ya mfumo unaohitajika kutumika kwa mujibu wa matakwa ya kazi zao ili kunusuru uwepo wa mifumo mingi ambayo haifanyi kazi ipasavyo na kupelekea matumizi mabaya ya fedha za Umma kwa kuanzisha mifumo mingi isiyokuwa na tija.

2.1.8 Kukosekana kwa mikataba ya mifumo ya TEHAMA (ZITAS, ERP SYSTEM na SAGE PASTEL Accounting Package)

Ukaguzi umeshindwa kupata mikataba halisi ya utengenezaji na usimamizi wa mifumo ya

TEHAMA ya Bodi ya Mapato Zanzibar. Mifumo ambayo imekosekana mikataba yake ni kama ifuatayo:-

- Zanzibar Integrated Tax Managemen System.
- Enterprise Resource Planning.
- Sage Pastel Accounting Package.

Kutokana na kutopata mikataba ya mifumo hiyo ukaguzi umeshindwa kupata taarifa kuhusiana na sheria na masharti yaliyowekwa kwenye mikataba pamoja na thamani halisi ya ununuzi wa mifumo hiyo jambo ambalo limepelekea kutopatikana kwa tija iliyokusudiwa kutokana na mifumo hiyo kukosa ufanisi katika utoaji wa huduma na kukusanya mapato.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuandaa na kuhifadhi vizuri mikataba ambayo Bodi inaingia na Kampuni nyengine kwa ajili ya kupata huduma mbali mbali. Aidha mikataba hiyo iweze kupatikana kwa wakati endapo ikihitajika.

2.1.9 Dosari katika Mfumo wa Enterprise Resource Planning (ERP)

Bodi ya Mapato Zanzibar imefanya manunuzi ya mfumo unaojulikana kwa jina Enterprise Resource Planning kwa ajili ya kuendesha kazi za mapato yasiyo ya kodi ikiwemo masuala ya fedha, malipo ya mishahara na rasilimali watu, mali za kudumu, usimamizi wa hati na nyaraka pamoja na manunuzi kupitia mitandao.

Ukaguzi haukuweza kupata mikataba wa manunuzi ya programu hiyo na kupelekea kushindwa kutoa maoni kuhusiana na mikataba huo.

Hata hivyo ukaguzi umebaini baadhi ya moduli za programu hiyo hazifanyi kazi ipasavyo ikiwemo moduli ya malipo ambapo imepeleleka kitengo cha Malipo kutumia programu za zamani kwa ajili ya malipo ya mishahara kwa wafanyakazi. baadhi ya moduli hazitumiki kabisa katika mfumo huo kama vile moduli ya Mali zisizohamishika, moduli ya Rasilimali watu , moduli ya usimamizi wa nyaraka na hati.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar haipati huduma za msaada wa kiufundi kutoka kwa Muuzaji wa Mfumo huo wa ERP (Vendor) na kupelekea kuibuka kwa changamoto nyingi katika mfumo huo.

Kutokana na kasoro zilizotajwa hapo juu ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuchukuwa jitihada za makusudi kuweza kufuatilia na kufanya Upembuzi Yakinifu wa kina kabla ya kuanzisha miradi ya kutengeneza mifumo pamoja na kuunda kamati Tendaji ya TEHAMA iliyo imara ili kuweza kutoa maamuzi sahihi na kuweza kuepukana na hasara zinazoweza kujitokeza kutokana na gharama kubwa zitakazotumika katika utengenezaji wa mifumo ambayo haitakuwa na ufanisi na tija katika utekelezaji wake.

2.1.10 Kukosekana kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa "Business Continuity Plan and Disaster Recovery Plan".

Utaratibu uliobora pamoja na miongozo ya kimataifa (ISO 22301) inahitaji Taasisi zenye huduma kupitia mifumo ya TEHAMA kuweka Mpango maalum wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona maafa (BCP & DRP).

Mpango huu ni muhimu na unasaidia taasisi kuendelea kutoa huduma za biashara na kuweza kupona maafa yanayoweza kutokezea endapo janga likitokea katika taasisi.

Mpango huo hutayarishwa kupitia miongozo inayoandaliwa na kutengenezewa hati/nyaraka ambazo zitathibitishwa na Uongozi wa Taasisi. Aidha taasisi inatakiwa kuweka miundombinu madhubuti ambayo itaweza kuhifadhi taarifa katika sehemu nyengine iliyo na umbali wa masafa kutoka sehemu kuu ya kuhifadhia taarifa (Disaster Recovery Site).

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar haina Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa. Aidha ZRB haijaweka miundombinu sehemu nyengine (Disaster Recovery Site) kwa ajili ya kuhifadhia taarifa endapo janga likitokea katika Ofisi kuu iliyopo Mazizini.

Kukosekana kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa kunaweza kusababisha upotevu mkubwa wa taarifa katika Bodi endapo janga likitokea.

Ukaguzi unashauri Bodi kuandaa Mpango mzuri wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa ikiwemo kuandaa sehemu maalum iliyo na umbali wa masafa kwa ajili ya kuhifadhia taarifa (Disaster Recovery Site).

2.1.11 Kukosekana kwa mafunzo endelevu kwa wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA cha Bodi ya Mapato Zanzibar

Moja ya majukumu ya wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA katika Bodi ya Mapato ni kusimamia na kutoa msaada wa kiufundi (technical support) kwa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA pamoja na mifumo iliyopo Bodi ya Mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA hawapati mafunzo ya mara kwa mara kuhusiana na usimamizi na utoaji wa msaada wa kiufundi wa mifumo ya TEHAMA iliyopo katika Bodi.

Kutokupata mafunzo ya mara kwa mara ya Usimamizi na utoaji wa msaada wa kiufundi wa mifumo ya TEHAMA kunaweza kupelekea kukosekana kwa huduma bora na zisizo na tija na hatimae kusababisha upotevu wa mapato kwa Serikali.

2.1.12 Dosari zilizobainika katika Kituo cha Taarifa (Datacenter) - PEMBA

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika Kituo cha Taarifa (Datacenter) cha Bodi ya Mapato kilichopo Tawi la Chake Chake - Pemba. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa vifaa madhubuti vya kuhifadhia umeme (High Power Backup - UPS) kwa ajili ya kuendesha miundombinu ya mawasiliano endapo umeme wa ZECO ukikatika.
- Kukosekana kwa jenereta la ofisi ambalo litatutumika kurejesha umeme endapo ukikatika.
- Kutotumika kwa Seva mbili ambazo zimenunuliwa karibuni kwa ajili ya matumizi ya kazi za Bodi.
- Chumba cha Seva ni kidogo na kimewekwa vifaa vingi vya kompyuta ambavyo vya zamani na havitumiki tena (ghala ya kuhifadhia kompyuta mbovu).
- Kukosekana kwa miundombinu ya kufanyia nakala (backup) za taarifa za Bodi.
- Kukosekana kwa mashine ambazo zitaweza kudhibiti kuingia wasiohusika pamoja na kuweka kumbukumbu za uingiaji ndani ya Chumba cha Seva (Fingerprints Scanners).
- Kukosekana kwa vifaa au mfumo wa kuzima moto endapo janga la moto likitokea.

Kasoro hizo zinaweza kupelekea upotevu na uharibikaji wa taarifa. Ukaguzi unashauri Bodi ya Mapato kufuatilia na kuzifanyia marekebisho ya dosari zinazojitokeza katika tawi la Ofisi ya Pemba.

2.1.13 Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu.

Bodi ya Mapato Zanzibar imefanikiwa kuongeza mchakato wa utoaji wa huduma za ukusanyaji wa kodi, utoaji wa leseni n.k katika matawi mbali mbali ya kwa Unguja na Pemba.

Kwa upande wa Pemba Bodi ya Mapato Zanzibar ina vituo sita vya utoaji wa huduma. Kati ya hivyo, vituo viwili (2) vikubwa ambavyo vipo Chake Chake na Wete na vituo vinne (4) vidogo ambavyo vipo Uwanja wa Ndege, Wete Bandarini, Mkoani na Weshi.

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato – tawi la Pemba kwa sasa kuna mfanyakazi mmoja tu katika kitengo cha TEHAMA ambaye anashughulikia vituo vyote sita vilivyopo Pemba kwa kusaidia kutatua changamoto za kiufundi kwa watoa huduma wote walioko vituoni.

Aidha ukaguzi umebaini mfanyakazi huyo kupewa majukumu yasiyoshabihiana na TEHAMA kama vile utoaji wa leseni za njia, utoaji wa leseni za magari, kusajili walipa kodi n.k.

Kufanya hivyo kunapelekea kuongezeka kwa majukumu ya kazi na kupungua kwa ufanisi wa utendaji kazi kwa wafanyakazi wa taasisi.

Hivyo ukaguzi unashauri Bodi ya Mapato kwa upande wa Pemba kuongeza idadi ya wafanyakazi katika kitengo cha TEHAMA ili kuweza kufanyika kazi hizo kwa ufanisi na uweledi.

2.1.14 Umiliki wa haki za matumizi ya kanzidata kwa wasiohusika.

Utaratibu uliobora unahitaji Uongozi wa Taasisi kulinda na kuhifadhi haki zote za matumizi ya mfumo na kanzidata zake na kutoa ruhusa ya matumizi kwa watu au taasisi maalum zilizo nje kuweza kutumia mfumo huo. Ili Kudhibiti Matumizi mbaya na kuepukana na Upotevu wa taarifa.

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar imetoa haki za matumizi ya mfumo kwa wauzaji wa mfumo. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea hatari ya kupotea kwa taarifa za Bodi ya Mapato, aidha kunaweza kupelekea kuvuja kwa siri kutokana na matumizi mabaya kwa wasiohusika.

SURA YA TATU

3.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO MKUU WA USIMAMIZI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR - PBZ

3.1 UTANGULIZI

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ilianzishwa tarehe 30 Juni 1966 na baadae kufanywa Shirika la Serikali chini ya Sheria ya Kampuni ya Zanzibar nambari 15 ya 2013 kama benki inayomilikiwa kikamilifu na Serikali inayotoa huduma zote za kibenki za Kiislamu na za kawaida. Benki ya Watu wa Zanzibar imesajiliwa kama benki chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, 2006. Hivi sasa Benki ya Watu wa Zanzibar ina matawi kumi na sita (16) na vituo vya Huduma vinne (4).

Benki ya Watu wa Zanzibar inatumia mfumo wa ICS BANKS (Core Banking System) ambao bado unafanyiwa maboresho ili kukidhi mahitaji ya Benki.

MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

Kasoro zilizobainika katika Utawala wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

3.1.1 Kukosekana kwa Mkataba wa Makubaliano ya kiwango cha utendaji (Operational Level Agreement – OLA)

Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa (ISO 20000), Benki inahitajika kuwa na nyaraka za Makubaliano (mkataba) yenye kuonesha malengo ya utekelezaji wa kazi za Idara ya TEHAMA ili kuendana na ufanisi wa utoaji huduma za kielektroniki za kibenki kwa wakati.

Mkataba huo wa Utendaji utaonesha mwongozo wa namna ya kutatua changamoto za kielektroniki zitakazojitokeza wakati mifumo ya TEHAMA inapotumika kwa watoa huduma pamoja na wateja.

Ukaguzi umebaini kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar haina mkataba rasmi wa Makubaliano ya Kiwango cha Utendaji kazi ambao utatumika katika kuamua kutoa huduma ambazo kitengo cha TEHAMA kitazitoa kwa watumiaji wa ndani ama wateja wa Benki.

3.1.2 Dosari katika Mpango wa Muendelezo wa Biashara (BCP) na Mpango wa Kupona Maafa (DRP)

Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa (ISO 22301) vinahitaji taasisi kuwa na Mpango wa Muendelezo wa Biashara pamoja na Mpango wa Kupona Maafa ili kuhakikisha rasilimali na Mifumo ya TEHAMA zinaendelea kufanya kazi kwa ufanisi endapo janga likitokea.

Ukaguzi umebaini kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar inatumia Mpango endelevu uliopitwa na wakati ambapo unajumuisha Mfumo Mkuu wa Kibenki (Bankers Realm Core Banking System) ambapo kwa sasa hautumiki tena.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar haina nyaraka za DRP kwa mujibu wa viwango vya kimataifa (ISO 22301) na Benki Kuu ya Tanzania (BOT).

- i. Ukaguzi haukuweza kupatiwa vielelezo vinavyohibitisha kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar inafanya Uchambuzi wa Athari za Kibiashara (Business Impact Analysis - BIA) kwa kipindi cha Ukaguzi wetu.
- ii. Ukaguzi umebaini kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar haifanyi mapitio ya kumbukumbu za shughuli zinazofanywa kwenye mifumo (Audit trail).

Kutokuwa na Mpango endelevu wa Biashara pamoja na Mpango wa Mpango wa Kupona Maafa kunaweza kupelekea Benki ya Watu wa Zanzibar kushindwa kuendelea na utoaji wa huduma za kifedha endapo mifumo yao ya kielektroniki itakapopatwa na majanga.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuandaa Mpango Endelevu pamoja na Mpango wa Kukabiliana na Majanga ili kuhakikisha huduma zote zinazotolewa kupitia Mifumo ya TEHAMA zitaendelea kupatikana endapo mifumo hiyo itakapo kabiliana na majanga. Sambamba na hivyo, ukaguzi unashauri dosari zilizobainika zichukuliwe hatua ili kuhakikisha uekezaji wa Mifumo ya TEHAMA inaleta tija na ufanisi katika utowaji wa huduma za kibenki.

SURA YA NNE

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA BIASHARA SHIRIKA LA UMEME - ZECO

4.1 UTANGULIZI

Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) limeanzishwa kwa Sheria nambari 3 ya mwaka 2006 kuchukua nafasi ya lililokuwa Shirika la Mafuta na Umeme la Serikali. Shirika la Umeme Zanzibar linamilikiwa kikamilifu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar likiwa chini ya usimamizi wa Wizara inayohusika na Nishati. Shughuli kuu za Shirika la Umeme Zanzibar ni uzalishaji, ununuzi, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa umeme katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Shirika la Umeme Zanzibar linatumia mifumo ya TEHAMA katika shughuli zake kwa kutambua faida za mifumo hii katika kufikia malengo ya Shirika kwa wakati na kwa gharama nafuu. Mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Shirika la Umeme ni pamoja na mfumo wa SUPREMA ambao unatumika kwa ajili ya usimamizi wa mita za TUKUZA, mfumo wa EQUILLIUM unaotumika kwa ajili ya usimamizi wa mita za zamani za kufanya malipo baada ya kutumia umeme, na mfumo wa SAP unaotumiwa na Shirika kwa ajili ya Kusaidia utendaji kazi wa shughuli zake za ndani za kiofisi.

MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

Katika ukaguzi uliofanyika wa mifumo ya TEHAMA ya Shirika la Umeme Zanzibar dosari zifuatazo zimebainika:-

4.1.1 Dosari katika uhakiki wa haki za watumiaji wa Mfumo wa SAP

Baada ya kufanya uhakiki wa watumiaji wa Mfumo wa SAP katika Shirika la Umeme, ukaguzi umebaini kwamba muuzaji wa mfumo wa SAP bado ana uwezo wa kuingia katika Mfumo pamoja na kanzidata (database) ya mfumo huo wakati anapohitaji bila ya kudhibitiwa na Shirika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Kimataifa vya usimamizi wa ulinzi wa taarifa za mifumo (ISO 27001) ambapo kunapelekea kuhatarisha usalama wa taarifa za Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuimarisha mipangilio ya haki za mfumo kwa kumzuia muuzaji wa mfumo huo asiwe na uwezo wa kuingia kwenye Kanzidata ya Shirika isipokuwa watakapohitaji kufanya hivyo.

4.1.2 Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu kwa watumiaji wa Mfumo

Utaratibu uliobora unahitaji kuwepo kwa mpango maalum wa mgawanyo wa majukumu ndani ya mfumo ambapo kila mtumiaji aliyesajiliwa anapewa haki ya kufanya miamala anayostahiki kwa mujibu wa muongozo wa majukumu yake.

Baada ya kupitia Mfumo wa SAP katika moduli mbali mbali kama vile Moduli ya uhasibu, ukaguzi umebaini kwamba maafisa wa kitengo cha TEHAMA wana ruhusa ya kuweza kuona, kufuta, kuongeza pamoja na kuwatoa watumiaji bila ya idhini ya Meneja Mkuu wa Fedha ambae kimsingi ndio mwenye dhamana ya taarifa za mfumo (Data owner).

Kufanya hivyo kunaweza kuhatarisha usalama wa taarifa za Shirika kwa kufanyiwa mabadiliko bila ya kuidhinishwa.

Aidha, baada ya kupitia Mfumo wa "Suprema" imebainika kwamba Mshika fedha Mkuu hakupewa uwezo wa kuzifatilia shughuli za washika fedha wanaohudumia wateja dirishani (teller) ili kuweza kuwasaidia katika zoezi la kufanya usuluhishi wa kifedha kila baada ya kukamilika mauzo ya kila siku kama ilivyo kwenye miongozo yake ya kazi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya majukumu ya kazi na kunaweza kupelekea shirika kuingia kwenye hasara ya upotevu wa fedha za mapato.

Ukaguzi unashauri Shirika la Umeme Zanzibar kuandaa mpango rasmi wa mgawanyo wa majukumu ndani ya mifumo yake kwa lengo la kuimarisha udhibiti ili kuepusha hasara zitokanazo na matumizi mabaya ya mifumo.

4.1.3 Kutokuwepo kwa Kamati ya Uendeshaji wa TEHAMA

Kwa mujibu wa muongozo wa usimamizi wa rasilimali za TEHAMA (COBIT-5 Framework) unazitaka taasisi kuwa na Kamati ya Uendeshaji wa Mifumo ya TEHAMA. Kamati hiyo ina jukumu la kusimamia utendaji wa mifumo ili kuhakikisha matumizi ya mifumo inakwenda sambamba na malengo ya taasisi katika kuimarisha ufanisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Umeme Zanzibar halijaanzisha Kamati ya Usimamizi wa TEHAMA licha ya kuwa na mifumo mbali mbali inayosaidia kuendesha shughuli za Shirika.

Kukosekana kwa Kamati ya Uendeshaji wa TEHAMA kunapelekea Shirika la Umeme kushindwa kusimamia vizuri uwekezaji wa shughuli za TEHAMA lakini pia shirika litashindwa kupima ufanisi wa mifumo katika kutimiza malengo waliojiwekea.

Ukaguzi unashauri Shirika la Umeme Zanzibar kuanzisha Kamati Tendaji ya TEHAMA kwa lengo la kusimamia mifumo na rasilimali za kompyuta.

4.1.4 Kutokutumia kwa Mfumo wa SAP Kikamilifu USD 65,000.

Ukaguzi umebaini kwamba mwaka 2005 Shirika la Umeme limetumia jumla ya dola za kimarekani 65,000 kwa ajili ya ununuzi na uwekaji wa mfumo wa kompyuta (software) unaojulikana kwa jina la SAP-ERP kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa shughuli za uhasibu, ununuzi, utunzaji wa mali za kudumu pamoja na usimamizi wa rasilimali watu.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba kitengo cha uhasibu bado kinafanya kazi za uhasibu kwa njia za utaratibu wa kawaida (manual) ambapo Mhasibu anatarisha hati za malipo na kuziingiza kwenye daftari la fedha taslimu na hatimae taarifa kuziweka kwenye leja kuu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Uhasibu wa Shirika kifungu nambari 17.1 ambapo kinaelekeza taarifa za hesabu zote zitokane na Mfumo wa SAP.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha wanaendelea kutumia mfumo wa SAP kama ilivyokusudiwa ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao.

SURA YA TANO

5.0 RIPOTI YA MFUMO WA USIMAMIZI WA TAARIFA NA MICHANGO YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII - ZSSF

5.1 UTANGULIZI

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) umeanzishwa kwa sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii nambari 2 ya 1998. Kabla ya kutungwa kwa Sheria hiyo na kuanzishwa kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, hakukuwa na mpango rasmi wa hifadhi ya jamii Zanzibar. Kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, wafanyakazi wa utumishi wa umma Zanzibar walikuwa wakipokea mafao ya pensheni chini ya Sheria ya Pensheni Nambari 2 ya 1990.

Katika kuboresha utendaji kazi wa Mfumo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wanachama, ZSSF inatumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA ikiwemo Mifumo ya Usimamizi wa Taarifa na Michango ya Wanachama (FUMIS na MIMS), Mfumo wa Usimamizi wa Michango ya Hiari (VOMIS) na Mfumo wa Usimamizi wa Masuala ya Fedha (Microsoft Navision).

MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

Katika ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) dosari zifuatazo zimebainika:-

5.1.1 Dosari katika kutoa haki za watumiaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya usimamizi wa ulinzi wa taarifa za mifumo (ISO 27001) pamoja na kifungu nambari 2.4.4 cha sera ya TEHAMA ya ZSSF kinahitaji kuwepo na mpango wa kuhakiki haki za watumiaji wa Mifumo ya TEHAMA mara kwa mara ili kuhakikisha watumiaji wa mifumo hawapati fursa ya kuona taarifa wasizostahiki au kufanya miamala isiyoidhinishwa (unauthorized access).

Ukaguzi umebaini kwamba Afisa wa Idara ya Uwekezaji amepewa haki isiyostahiki ya kuingiza na kuona taarifa za hati ya malipo kwenye Kifurushi cha Mfumo wa "Microsoft Navision". Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sera za TEHAMA za ZSSF.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kubainisha muda maalum katika sera ya TEHAMA kwa ajili ya kufanya uhakiki wa haki za watumiaji wa Mifumo mara kwa mara ili kuhakikisha kila mtumiaji wa Mfumo anapata ruhusa ya kufanya miamala anayostahiki kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu.

5.1.2 Dosari katika Usimamizi wa mabadiliko ya Programu za Kompyuta

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) umefanya mabadiliko mbali mbali katika Mfumo wa "Microsoft Navision" ili kuhakikisha

mfumo huo unaendana na mahitaji ya kazi zao.

Ukaguzi umebaini kwamba ZSSF haikufuata utaratibu maalum wa kusimamia mabadiliko ya mifumo ikiwemo kutokujaza fomu za maombi ya mabadiliko na kutokuidhinishwa kwa mabadiliko hayo na Kamati Tendaji ya TEHAMA pamoja na taratibu nyengine kama ilivyoelekezwa katika sera ya TEHAMA kifungu nambari 2.3.4.

Kufanya mabadiliko ya Mifumo bila ya kuwa na udhibiti maalum kunapelekea kupata toleo la Mfumo ambao hautoleta tija na ufanisi katika utendaji wa kazi zake.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa ZSSF kufuata taratibu sahihi katika kufanya mabadiliko ya mifumo kama ilivyoelekezwa katika sera ya TEHAMA pamoja na kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya usimamizi wa ubora wa mfumo (ISO 9001:2015).

5.1.3 Kutofanyika zoezi la majaribio ya Taarifa mbadala (backup data restoration test)

Katika kuhakikisha mifumo inaendelea kusimamia shughuli za kibiashara wakati wote, utaratibu uliobora ni kufanya zoezi la kuweka taarifa mbadala (backup data) pamoja na kuzifanyia majaribio.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) unaweka taarifa mbadala kwa kila siku na kuzihifadhi kwenye kifaa cha kuntunzia taarifa (hard disk). Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuzifanyia majaribio taarifa mbadala ili kubaini usahihi wake kwa ajili ya matumizi ya baadae wakati zitakapo hitajika. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba kifaa kinachotumika kutunzia taarifa mbadala (hard disk) inawekwa kwenye chumba cha seva kilichopo ndani ya jengo la ZSSF.

Kutokufanya majaribio ya taarifa mbadala kunapelekea kushindwa kubaini usahihi na uwiano wa taarifa zilizohifadhiwa na hatimae kusababisha kutokea upotevu wa taarifa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kufanya zoezi la majaribio ya taarifa mbadala pamoja na kuwa na eneo maalum la nje kwa ajili ya kuhifadhi taarifa mbadala (Offsite backup location) ili kutofautisha taarifa mbadala na zile taarifa zilizopo kwenye mazingira ya uzalishaji (Production data).

5.1.4 Dosari katika utekelezaji wa Mpango wa Kupona Maafa (DRP)

Katika kuhakikisha huduma za kibiashara zinaendelea kutolewa kupitia Mifumo ya TEHAMA utaratibu uliobora kupitia viwango vya kimataifa (ISO 22301) unazitaka taasisi kuwa na Mpango wa Kurejesha Huduma baada ya kutokezea Majanga (DRP).

Ukaguzi umebaini kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) unao Mpango wa Kurejesha Huduma baada ya kutokezea Majanga (DRP). Dosari iliyobainika ni kutokufanya majaribio ya mpango huo ili kuweza kuokoa taarifa endapo janga likotokea katika Ofisi.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa ZSSF kuhakikisha kuimarisha mpango huo na kufanya majaribio ya Mpango wa Kupona Maafa ili kuepusha athari zinazotokana na majanga.

MAPENDEKEZO

Kutokana na dosari mbali mbali zilizobainika katika Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatoa mapendekezo kwa taasisi zinazotumia mifumo ya TEHAMA kama ifuatavyo:-

- a) Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kwa niaba ya Serikali kuunganisha mifumo yao na Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Fedha za Serikali (IFMIS) kwa lengo la kupata Usimamizi mzuri mapato na matumizi ya fedha za Serikali.
- b) Kuhakikisha kwamba taasisi zinazotumia mifumo ya TEHAMA zinafuata Sera, Viwango na Miongozo ya matumizi ya mifumo iliyowekwa na Serikali (e-Gov).
- c) Kuhakikisha kwamba Taasisi zinazotumia mifumo ya TEHAMA zinaandaa miongozo mbali mbali ya TEHAMA itakayokwenda sambamba na sera za TEHAMA za Serikali na kusimamia utekelezaji wa miongozo hiyo.
- d) Kufanya upembuzi yakinifu (feasibility Study) kwa taasisi kabla ya kuanza kutengeneza mifumo ya TEHAMA.
- e) Kuongeza uelewa kwa Maafisa Wahasibu (Accounting Officers) pamoja na watumiaji wa Mifumo juu ya hatari zinazohusiana na matumizi ya TEHAMA.
- f) Kuhakikisha kwamba kunakuwa na utekelezaji mzuri wa mipango mikakati ya TEHAMA katika Taasisi.
- g) Kushirikisha watumiaji wa mifumo kuanzia hatua za awali za utengenezaji wa mifumo hadi kukamilika kwake.

VIAMBATISHO**KIAMBATISHO NAMBARI 1: Nambari za kumbukumbu za Hati za Exchequer zinazofanana kwa fedha zilizotolewa kwenda Mafungu Makuu tofauti ya Bajeti**

Tarehe	Nambari ya Kumbukumbu ya Mfumo wa IF-MIS	Wizara/Idara	Kumb. ya Benki	Kiasi Kilichoin-gizwa	Kifungu cha Bajeti
30-Nov-2018	19CR2186	Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda	DUMMY112018/INFRA	7,334,143.00	Dummy Development Exchequer - DD
30-Nov-2018	19CR2186	KMKM	DUMMY112018/INFRA	299,930,612.00	Dummy Development Exchequer - DD
30-Nov-2018	19CR2186	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	DUMMY112018/INFRA	12,001,000.00	Dummy Development Exchequer - DD
30-Nov-2018	19CR2186	Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	DUMMY112018/INFRA	1,719,722,930.00	Dummy Development Exchequer - DD
23-Jul-2018	19CR1992	Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Wanawake na Watoto	MOFB1018075	35,817,500.00	Development Partner (DP)1
23-Jul-2018	19CR1992	Wizara ya Afya	MOFB1018075	89,734,600.00	Development Partner (DP)1
31-Jul-2018	19CR2008	Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Wanawake na Watoto	MOFPB10180712	200,000,000.00	Development Contribution (DC)1
31-Jul-2018	19CR2008	KMKM	MOFPB10180712	230,000,000.00	Development Contribution (DC)1
31-Jul-2018	19CR2008	Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Uvuvi	MOFPB10180712	382,000,000.00	Development Contribution (DC)1
31-Jul-2018	19CR2008	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	MOFPB10180712	22,000,000.00	Development Contribution (DC)1
31-Jul-2018	19CR2008	Tume ya Mipango	MOFPB10180712	130,000,000.00	Development Contribution (DC)1

31-Jul-2018	19CR2008	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	MOFPB10180712	450,000,000.00	Development Contribution (DC)1
31-Jul-2018	19CR2008	Ofisi ya Rais Fedha na Mipango	MOFPB10180712	1,500,000,000.00	Development Contribution (DC)1
28-Feb-2019	19CR2306	Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati	DUMMY022019/INFRA	659,009,848.33	Dummy Development Exchequer - DD
28-Feb-2019	19CR2306	Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda	DUMMY022019/INFRA	41,875,349.98	Dummy Development Exchequer - DD
28-Feb-2019	19CR2306	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	DUMMY022019/INFRA	24,001,999.98	Dummy Development Exchequer - DD
28-Feb-2019	19CR2306	Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	DUMMY022019/INFRA	1,749,750,999.99	Dummy Development Exchequer - DD
28-Feb-2019	19CR2307	Ofisi ya Rais Fedha na Mipango	DUMMY022019/INFR	25,000.00	Dummy Development Exchequer - DD
29-Mar-2019	19CR2357	Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati	DUMMY032019INFRA	931,475,026.43	Dummy Development Exchequer - DD
29-Mar-2019	19CR2357	Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda	DUMMY032019INFRA	2,258,025.00	Dummy Development Exchequer - DD
29-Mar-2019	19CR2357	Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	DUMMY032019INFRA	2,732,500,988.99	Dummy Development Exchequer - DD
29-Apr-2019	19CR2387	Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda	DUMMY042019INFRA	120,011,999.98	Dummy Development Exchequer - DD
29-Apr-2019	19CR2387	KMKM	DUMMY042019INFRA	75,083,740.61	Dummy Development Exchequer - DD
29-Apr-2019	19CR2387	Wizara ya Afya	DUMMY042019INFRA	321,188,596.30	Dummy Development Exchequer - DD

29-Apr-2019	19CR2387	Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	DUMMY042019INFRA	1,732,500,999.99	Dummy Development Exchequer - DD
29-Apr-2019	19CR2387	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na BLW	DUMMY042019INFRA	183,425,096.99	Dummy Development Exchequer - DD
20-Jan-2020	20CR2812	Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale	MOFPB10200108	357,707,480.00	Subvention Salary - SS1
20-Jan-2020	20CR2812	Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Wanawake na Watoto	MOFPB10200108	53,453,765.00	Subvention Salary - SS1
20-Jan-2020	20CR2812	Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati	MOFPB10200108	463,008,302.00	Subvention Salary - SS1
20-Jan-2020	20CR2812	Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda	MOFPB10200108	79,150,790.00	Subvention Salary - SS1
20-Jan-2020	20CR2812	Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo	MOFPB10200108	18,208,335.00	Subvention Salary - SS1
20-Jan-2020	20CR2812	Mahkama Kuu, Zanzibar	MOFPB10200108	67,584,505.00	Subvention Salary - SS1
18-Feb-2020	20CR2847	Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale	MOFPB10200209	359,572,530.00	Subvention Salary - SS1
18-Feb-2020	20CR2847	Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Wanawake na Watoto	MOFPB10200209	53,453,765.00	Subvention Salary - SS1
18-Feb-2020	20CR2847	Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati	MOFPB10200209	467,338,412.00	Subvention Salary - SS1

KIAMBATISHO NAMBARI 2 :

(a) Orodha wa watumiaji wa mifumo wenye utata (duplicated/ambiguous users), watumiaji wasiojulikana, watumiaji ambao taarifa zao hazieleweki pamoja na watumiaji ambao wapo likizo lakini akaunti zao za matumizi hazijafungwa kwenye mfumo.


User ID	User Name	User Disabled	Current Comp	Pwd Expires	Group List	Last Log On Attempt	Remarks
AHSANTEI6940	AHSANTE GHARIB BILAL	1	A04	13/10/2015	CA	2015-10-07 15:04:12.343	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
AHSANTEGB16940	AHSANTE GHARIB BILAL.	0	N02	19/03/2021	CA	2021-03-02 09:08:05.383	
AKHAMIS	Khamis Ali Khamis	1	0	01/02/2016	BG~EO~ImpAd- mGrp~JA~Rec~C- PO-T~EA~AA~EX- ~DE~RO~CPO~IMPACC~ CA~PMU~SA	2016-04-12 10:51:49.260	Mtumiaji asie na Payroll Number (unknown user)
ALIKM07658	ALI KHAMIS MWINYI	1	D01	15/10/2015		2015-07-17 11:04:15.797	Mtumiaji haeleweki katika taarifa zake za userID na Username.
AIKIM807658	ALI KHATIB MWINYI	1	D01	P	CA	2020-03-16 16:01:15.247	
AminAY47612	AMINA ALAWI YUSSUF	1	J02	03/03/2016	CA	2016-02-03 10:51:28.587	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
AminAY547612	AMINA ALAWI YUSSUF	1	J02	29/10/2019	REVENUE	2019-07-31 09:44:33.460	
Aminam	AMINA MOHAMMED KHAMIS	0	0	14/03/2021	VENDOR~CORE APP	2021-03-01 14:52:23.283	Mtumiaji asie na Payroll number (unknown user)

AYAHYA	Asha Yahya Hamad	0	J04	31/05/2021	BG~EO~CA~ImpAd- mGrp~IA~EO~A~Rec~C- PO~T~REVENUE~VEN- DOR~EA~EX~DE~RO~AP- PR~PMU~CORE APP~CPO~IMPAC- C~AA~BG~A~PMU~SA	2021-03-02 15:01:25.943	Mtumiaji asie na Payroll number (unknown user)
BAKARISB49145	BAKAR SHAABAN BAKAR	1	B01	06/04/2017	DE	2017-01-06 14:12:40.533	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
BakarSB749145	BAKAR SHAABAN BAKAR.	1	0	18/10/2020	CPO	2020-09-02 15:24:06.967	
CA	Chief Accountant	0	A01	NULL	CA	NULL	
FatmaSM755496	FATMA SEIF MOHD	0	0	23/05/2021	Rec	2021-03-02 06:52:15.563	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
FATMASS755496	FATMA SEIF MOHD	1	0	29/10/2015	CPO	2019-02-27 10:41:16.427	
IddiHH148492	IDDI H HAMAD	1	H01	23/02/2020	DE	2020-01-27 11:22:40.557	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
IDDIHH48492	IDDI HASSAN HAMAD	1	G01	14/04/2020	DE	NULL	
Ifmuser	Ifmuser	1	0	NULL		2016-04-13 08:56:31.630	Mtumiaji asiejulikana (unknown user).
JamiliaMH00006001	JAMILA MOHD HAJI	1	J01	16/09/2020	REVENUE	NULL	Mtumiaji mwenye payroll number yenye shaka.
Khadjam	Khadija Mohamed Ahmed	1	F01	19/01/2016	BG~EO~ImpAd- mGrp~IA~Rec~EA~AA~EX- ~DE~RO~CPO~IMPACC~ CA~PMU~SA	2016-05-20 14:17:37.780	Mtumiaji asie na Payroll number (unknown user)


KOMBOKK47573	KOMBO KHAMIS KOMBO	1	E01	27/05/2019	DE	NULL	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
Kombokk647573	KOMBO KHAMIS KOMBO	0	F01	12/05/2021	DE	2021-03-01 15:40:41.780	
Manager	System Manager	0	0	NULL	BG~CPO~T~EO~ACC~ImpA dmGp~DE~JA~Rec~CPO~ RO~AA~EX~CA~EA~IMPAC C~PMU~SA	2021-03-02 15:01:35.960	Mtumiaji asiejulikana (unknown user)
MaryamBM400022	Maryam Bushir Mahmoud	0	0	19/04/2021	VENDOR~DE	2021-02-22 08:19:28.060	Mtumiaji ambae yupo likizo lakini akaunti yake haijazuwiwa.
MWANTATU	MWANTATU FADHIL KHAMIS	1	B01	24/10/2016	RO	2016-07-26 11:31:57.287	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated/ ambiguous user)
MwantatuFK913417	MWANTATU FADHIL KHAMIS.	0	0	14/03/2021	BG~EO~ACC~Impad- mGp~JA~EO~A~Rec~C- PO~T~RO~REVE- NUE~AA~EX~DE~EA~APPR PMU~CORE APP	2021-03-02 15:01:28.507	
Print	Print for task agent	0	0	NULL		2021-03-02 15:03:15.147	Mtumiaji asiejulikana (unknown user)
RukiaAS107732	Rukia A Salmin	0	F02	16/05/2021	CA~VENDOR	2021-03-02 14:39:58.550	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated user)
RukiaAS412870	Rukia A. Salmin	1	F02	15/12/2019	CA	2019-10-17 09:11:27.957	
SALMAMS246962	SALMA MOHD SAID	1	H01	NULL	DE	2019-05-24 09:51:12.997	Mtumiaji mmoja mwenye UserID mbili (duplicated user)
SALMAMS5715	SALAM MOHD SAID	0	H01	07/12/2018	DE	NULL	
SHIRAZISS745808	SHIRAZI SEIF SALUM	0	E04	24/09/2018	DE	NULL	Mtumiaji ambae yupo likizo lakini akaunti yake haijazuwiwa.
Webaccess	Webaccess	0	XXX	NULL		2015-02-12 15:53:53.017	Mtumiaji asiejulikana (unknown user)


(b)Kutumika kwa Akaunti Asili "Default Accounts " za wasimamizi wa Mfumo wa IFMIS.

(c) Seva ya uzalishaji ambayo Mfumo wake wa Uendeshaji wa "Operating System" hauna leseni ya matumzi.




(d)Kasoro zilizobainika katika Kudhibiti matumizi ya Mtandao wa Internet, Programu, Kompyuta na Media.





(e) Baadhi ya Kompyuta za IFMIS ambazo zinatumia programu ya kuweka usalama (Antivirus) zilizokuwa hazina leseni.



(f) Kompyuta za IFMIS zinazotumia Mfumo wa zamani wa uendeshaji wa kompyuta ambao ushapitwa na wakati na hauko salama kwa matumizi (Windows 7 Operating System).



